**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,**

**WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# MWONGOZO WA TAIFA WA UENDESHAJI MAJADILIANO KUHUSIANA NA MILA NA DESTURI ZENYE MADHARA KWA JAMII

**APRILI, 2022**

## YALIYOMO

**DIBAJI…………………………………………………….....vi**

**SHUKRANI………………………………………….….ix**

**FASILI YA DHANA ZA MSINGI……………………......xi**

**ORODHA YA VIFUPISHO……………………….......xvi**

**SURA YA KWANZA……………………………………...1**

**MWONGOZO WA MAJADILIANO KUHUSIANA NA MILA NA DESTURI YENYE MADHARA KWENYE JAMII……………………………………………………..…1**

1.1. Utangulizi……………………………………………..1

1.2.Umuhimu wa Mwongozo……………………………2

1.3.Lengo Kuu……………………………………………4

1.4. Malengo Mahsusi……………………………….…4

1.5. Watumiaji wa Mwongozo wa Majadiliano Ngazi ya Jamii……………………………………………………..5

1.6. Majukumu na Wajibu wa Wadau…………………...6

1.6.1. Ngazi ya Wizara……………………………………6

1.6.2. Ngazi ya Mkoa……………………………………..7

1.6.3. Ngazi ya Halmashauri……………………………..8

1.6.4. Ngazi ya Kata/Kijiji/Mtaa…………………………..9

1.6.5. Wadau……………………………………………..…10

1.6.6. Jamii…………………………………………...…..11

1.7. Mpangilio wa Mwongozo…………………………..……12

**SURA YA PILI……………………………………………...13**

**MAJADILIANO YA KIJAMII…………………………..…..13**

2.1. Majadiliano Ngazi ya Jamii ni nini?......................13

2.2. Manufaa ya Majadiliano…………………………...14

2.3. Malengo ya Majadiliano Ngazi ya Jamii…………15

2.4. Changamoto za Majadiliano Ngazi ya Jamii…….16

2.5. Kanuni Muhimu……………………………….…17

2.5.1. Umuhimu wa Kuwa Makini katika Masuala ya Kijinsia…………………………………………………..…...17

2.5.2.Kulinda na Kuepusha Madhara………………...17

**SURA YA TATU…………………………………………...19**

**MWONGOZO KWA WAWEZESHAJI………………...19**

3.1. Mbinu za Uwezeshaji……………………………..…..19

3.2. Mbinu za Ujifunzaji kwa Watu Wazima…………..20

3.3. Stadi Shirikishi za Kujifunza………………………21

3.4. Miiko na Maadili ya Mwezeshaji…………………..22

3.5. Mbinu za Uwezeshaji Zilizochaguliwa…………....28

3.5.1. Mbinu ya Kujifunzia Kuzingatia Kiini cha Tatizo………………………………………………………...28

3.5.2. Majadiliano ya Wazi…………………………….....30

3.5.3. Majadiliano ya Kikundi…………………………...31
3.5.4. Majadiliano ya Kikundi Lengwa…………………31
3.5.5. Igizo……………………………………………..32
3.5.6. Bungua Bongo…………………………………32
3.5.7. Kisa Mkasa……………………………………..33
3.5.8. Mti wa Matatizo na Suluhisho…………………..33
3.5.9. Bakuli la Jinsia…………………………………34
3.5.10. Shughuli za Jinsi Moja………………………..…34

**SURA YA NNE…………………………………….….36**
**KUPANGA NA KUENDESHA MAJADILIANO YENYE UFANISI NGAZI YA JAMII……………………………..36**
4.1. Kupanga Majadiliano Ngazi ya Jamii…………….36
4.1.1. Itifaki za Kuzingatia Kabla ya Majadiliano……..36
4.1.2. Walengwa……………………………………….36
4.1.3. Utambulisho wa Mahali pa Kufanyia Majadiliano……………………………………………….38
4.1.4. Uteuzi wa Mbinu na Zana za Uwezeshaji……..40
4.1.5. Muda wa Majadiliano…………………………….40
4.1.6. Huduma Zinazopatikana………………………...41
4.1.7. Kukamilisha Maandalizi ya Mada za Kikao……41
4.2. Kuendesha Majadiliano Ngazi ya Jamii…………42

4.2.1. Kuwasili, Kujiandikisha na Kuketi………………42
4.2.2. Kuanza Majadiliano………………………………43
4.2.3. Kuanzisha Ajenda na Mbinu za Majadiliano…..44
4.2.4.Matarajio ya Washiriki na Kuunda Kanuni za Msingi……………………………………………………..45
4.2.5. Kuanza kwa Majadiliano…………………………46
4.2.6. Mpango Kazi wa Utekelezaji baada ya Majadiliano……………………………………………47
4.2.7. Itifaki ya Kuhitimisha Majadiliano……………….47
4.2.8. Ufuatiliaji na Kuendeleza Majadiliano…………48

**SURA YA TANO………………………………………...50**
**UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI……………………………………………..50**
5.1. Utunzaji wa Kumbukumbu za Majadiliano……….50
5.2. Kutathmini Matokeo………………………………..51
**VIAMBATISHO……………………………………….53**
**KIAMBATISHO NA. 1: MILA NA DESTURI ZITAKAZOHUSISHWA WAKATI WA MAJADILIANO YA JAMII ZINAZOSABABISHA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO…………………………...54**

**KIAMBATISHO NA. 2: MFANO WA UTARATIBU WA MAJADILIANO……………………………………………..55**

**KIAMBATISHO NA. 3: FOMU YA KUTOA TAARIFA YA MAJADILIANO NGAZI YA JAMII (FOMU NA. 1)………………………………..…………………..101**

**KIAMBATISHO NA. 4: FOMU YA MPANGO KAZI WA JAMII (FOMU NA. 2)………………………………..…103**

**KIAMBATISHO NA. 5: TATHMINI KABLA NA BAADA YA MAJADILIANO……………………......................104**

# DIBAJI

Mwaka 2016, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ili kushughulikia, pamoja na mambo mengine, mila na desturi zenye kuleta madhara ikiwemo; ukeketaji, ndoa za utotoni, mimba za utotoni, pamoja na desturi za malezi zinazochochea ukatili wa kimwili na kihisia dhidi ya wanawake na watoto au unaosababisha kesi za ukatili kutokutolewa taarifa. Mpango huo unalenga kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2021/22.

Ili kufanikisha hilo, mpango uliandaliwa kwa kujikita katika Maeneo ya Utekelezaji nane (8) ambapo mojawapo ya maeneo hayo ni Mila na Desturi. Mpango huo umeainisha afua mbalimbali kupitia Maeneo ya Utekelezaji zinazolenga kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Miongoni mwa afua hizo ni kuandaa mikakati na miongozo ikiwemo Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi Zenye Madhara Kwa Jamii ili kutoa mchango katika kutekeleza azma ya kutokomeza aina zote za ukatili ikiwa ni pamoja na ukatili unaosababishwa na mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii.

Mwongozo umeandaliwa ili kuhakikisha matumizi ya mbinu bora katika uendeshaji wa majadiliano kuhusu

umuhimu wa kuendeleza mila na desturi chanya na kutokomeza zile zenye kuleta madhara kwenye jamii na zinazozorotesha jitihada za kufikia usawa wa kijinsia, ukiukwaji wa haki za wanawake na wasichana na hivyo kuzuia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mwongozo unatumia mbinu shirikishi ambayo inaruhusu wanajamii wote kupaza sauti zao kuhusu imani, hofu, mila na desturi zinazoendeleza ukatili ikiwa ni pamoja na ukeketaji, ndoa za utotoni na mimba za utotoni. Kwa kuzingatia hayo, Mwongozo unatoa mbinu za kuwezesha jamii kuelewa kwa kina mila na desturi zenye kuleta madhara na jamii kuwa na fikra na mitazamo chanya katika kutambua hatua zinazohitajika kuchukuliwa katika ngazi ya jamii ili kuleta mabadiliko ya kweli na stahimilivu.

Hivyo, ili kukabiliana na changamoto za mimba na ndoa za utotoni pamoja na tatizo la ukeketaji nchini, Mwongozo utatumia mifano, ushahidi, uzoefu pamoja na masuala muhimu ya kujifunza ikiwemo mifano bora ya kuigwa kutoka ndani ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupunguza changamoto hizo. Utekelezaji wa Mwongzo utafanyika kwa kutumia mbinu na mfumo mzima unaoshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Serikali, Sekta Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), Mashirika ya Kidini (FBOs), Mashirika ya Kijamii (CBOs),

wanafamilia, vyombo vya habari, wanawake, wanaume, wasichana, wavulana na jamii kwa ujumla.



Dkt. Zainab A.S. Chaula
**KATIBU MKUU**

## SHUKRANI

Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii umeandaliwa ili kuwezesha jamii kufanya majadiliano ya pamoja kuhusiana na mila na desturi chanya zinazotakiwa kuendelezwa na zile zenye kuleta madhara katika jamii zinazopaswa kutokomezwa ili kupunguza pengo la usawa wa kijinsia. Mwongozo umeandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WMJJWM) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na unalenga kuongeza chachu ya utekelezaji wa Eneo la Pili la Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Aidha, Mwongozo huu ni matokeo ya mashauriano ya kina yaliyofanywa na Serikali pamoja na Wadau wa Maendeleo katika eneo la mila na desturi.

WMJJWM inatoa shukrani zake za dhati kwa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) kwa kuchangia rasilimali fedha na utaalam ili kuwezesha maandalizi ya Mwongozo huu. Pia Wizara inatoa shukrani kwa  Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) kwa ushiriki wao katika kufanikisha maandalizi na ukamilishaji wa Mwongozo huu.

Aidha, WMJJWM inawashukuru wadau wote wakiwemo washirika wa utekelezaji ambao walihusika kwa karibu wakati wa mchakato wa maandalizi. Wadau hao ni pamoja na; Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji (IRC), Mashirika mbalimbali yakiwemo Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF), *Engender Health*, *Huruma Aids Concern and Care* (HACOCA), Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria Awamu ya Pili (LVEMP II), UZIKWASA - Pangani na *Community Focus on Teen and Single Mothers Welfare* (CFTSW).

Pongezi za pekee ziende kwa mwezeshaji kiongozi Dkt. Katanta M. Simwanza na wawezeshaji wenza Bw. Benny Muga Lugoe, Bw. Hamis Kiloya na Bw. Iddi Rajabu Mziray ambao walitoa mchango wa kitaalamu katika kuwezesha mikutano ya mashauriano ya wadau na ukamilishaji wa Mwongozo huu.

# FASILI YA DHANA ZA MSINGI

| | |
|---|---|
| **Desturi** | Imani za mtu binafsi zinazohamasisha watu kutenda kwa njia moja au nyingine. Hutumika kama mwongozo wa tabia ya mwanadamu. Baadhi ya desturi zina thamani ya ndani, kama vile upendo, ukweli na uhuru. Desturi zingine, kama vile tamaa, uwajibikaji, na ujasiri, huelezea sifa au tabia ambazo ni muhimu kama njia ya kufikia lengo. |
| **Kijana Balehe** | Mvulana au msichana mwenye umri kati ya miaka 10-19. |
| **Majadiliano Ngazi ya Jamii** | Afua zinazohusisha majadiliano ya pamoja, kubadilishana mawazo na uzoefu kuhusu maisha ya kila siku, uwiano wa kijamii, afya na ustawi wa jamii. Majadiliano huongozwa na mwezeshaji kufikia maelewano ya amani juu ya hatua ya pamoja ya kushughulikia mila na desturi hususan zile zenye madhara kimwili, kisaikolojia, kiafya na kiuchumi katika jamii |
| **Majadiliano yenye Ufanisi Ngazi ya Jamii** | Mchakato wa kimfumo unaolenga kupata maarifa chanya, kuboresha mtazamo na kuleta mabadiliko ya tabia dhidi ya mila na desturi hususan zile zenye madhara |

| | |
|---|---|
| | kimwili, kisaikolojia, kiafya na kiuchumi katika jamii. |
| **Malezi** | Mchakato wa kusaidia na kuwezesha maendeleo na ukuaji wa mtoto kimwili, kihisia, kijamii, kifedha na kiakili kutoka utoto hadi utu uzima. Hii inahusisha kulea mtoto bila kujali uhusiano wa kibaiolojia. |
| **Manusura** | Mtu (mtoto au mtu mzima, mwanamke au mwanaume) ambaye amenusurika kutokana na vitendo vya ukatili ikiwemo kimwili, kiuchumi, kingono na/au kisaikolojia kwa sababu ya jinsi yake. |
| **Mila** | Kanuni na matarajio ambayo hubainisha namna watu wanapaswa au wasivyopaswa kuishi katika hali mbalimbali za kijamii. Mila kwa hali ya kawaida ni za ndani lakini pia zinaweza kuathiriwa na mila za kigeni ambazo huasiliwa na jamii mara kwa mara. |
| **Mimba za Utotoni** | Hali ambayo msichana/mtoto wa kike anapata ujauzito akiwa katika umri wa chini ya miaka 18. |
| **Mtoto** | Mtu yeyote mwenye umri chini ya |

| | |
|---|---|
| | miaka 18. |
| **Mwendelezaji wa Vitendo vya Ukatili** | Mtu, kikundi au taasisi ambayo inasababisha, kuunga mkono, na/au kuchochea vitendo vya ukatili au aina nyingine za unyanyasaji dhidi ya mtu au kikundi cha watu. |
| **Mwezeshaji** | Mtu asiyeegemea upande wowote ambaye huratibu na kuiongoza jamii katika majadiliano juu ya mila na desturi zilizotambuliwa au masuala yanayohusiana ambayo yanahitaji ufumbuzi wa kudumu. |
| **Mzazi** | Baba au mama wa kibaiolojia, baba au mama mlezi kwa kuasili, na mtu mwingine yeyote ambaye mtoto amewekwa chini ya uangalizi wake. |
| **Ndoa ya Utotoni** | Muungano wowote ulio rasmi au usio rasmi ambapo mmoja au pande zote mbili zinahusisha watu wenye umri chini ya miaka 18. |
| **Ukatili** | Ni matumizi ya makusudi ya nguvu au uwezo wa kimwili kutishia au kufanya kitendo dhidi yako mwenyewe, mtu mwingine na/au dhidi ya kikundi au jamii ambayo yanaweza kusababisha au kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha majeraha, kifo, |

| | |
|---|---|
| | madhara ya kisaikolojia, kuzorotesha maendeleo na/au kunyimwa haki. |
| **Ukatili dhidi ya Wanawake** | Ni vitendo vyovyote vile vinavyofanywa na mtu au kikundi dhidi ya wanawake vinavyosababisha au vinavyoweza kusababisha madhara ya kimwili, kingono, kisaikolojia na kiuchumi, vikijumuisha vitisho au kumnyima mtu uhuru wa msingi katika maisha yake wakati wa amani au katika hali ya migogoro ya kivita. |
| **Ukatili dhidi ya Watoto** | Ni matumizi ya makusudi ya nguvu, vitisho vinavyofanywa na mtu au kikundi dhidi ya mtoto na kumsababishia kupata madhara ya kimwili, kiafya na kisaikolojia hivyo kuathiri maendeleo na utu wake. |
| **Ukatili kati ya Wenzi** | Tabia katika uhusiano wa mume na mke unaosababisha madhara ya kimwili, kingono au kisaikolojia ikijumuisha shambulio la kimwili, kumwingilia kimwili bila ridhaa yake, unyanyasaji wa kisaikolojia na kumnyima uhuru. |

| | |
|---|---|
| **Ukatili wa Kijinsia** | Hali ya unyanyasaji wa kimwili, kisaikolojia, kingono au kiuchumi unaofanywa na mtu mmoja dhidi ya mtu mwingine kwa kigezo cha jinsi yake. |
| **Ukeketaji** | Inajumuisha taratibu zote zinazohusisha uondoaji wa eneo dogo au kubwa la sehemu za siri za mwanamke au kusababisha majeraha mengine kwenye viungo vya uzazi vya mwanamke, au utaratibu wowote wenye madhara kwa sehemu za siri za mwanamke kwa sababu zisizo za kimatibabu. |
| **Unyanyasaji** | Ni ukiukwaji wa haki unaosababisha madhara ya kimwili, kiafya, kimaadili au kihisia ikiwa ni pamoja na kipigo, matusi, ubaguzi, utelekezaji na ukatili wa kingono. |
| **Utelekezaji wa Mtoto** | Hali ya mzazi au mlezi kushindwa kutoa ulinzi au uangalizi unaohitajika na kumpa huduma za msingi mtoto mathalani chakula, malazi, mavazi, elimu, uangalizi wa kiafya, n.k. |
| **Waathirika** | Watu ambao wameumizwa, wamejeruhiwa au kuuawa kwa sababu ya uhalifu, ajali au kitendo fulani ama tukio lingine. |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **CBOs** | Mashirika ya Kijamii |
| **CDF** | Jukwaa la Utu wa Mtoto |
| **CFTSW** | Community Focus on Teen and Single Mothers Welfare |
| **CSOs** | Asasi za Kiraia |
| **FBOs** | Mashirika ya Kidini |
| **FGM** | Ukeketaji |
| **GBV** | Ukatili wa Kijinsia |
| **HACOCA** | Huruma Aids Concern and Care |
| **HIV** | Virusi vya UKIMWI |
| **IRC** | Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji |
| **LVEMP II** | Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria Awamu ya Pili |
| **MTAKUWWA** | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto |
| **NGOs** | Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TDHS-MIS** | Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria |

| | |
|---|---|
| **TGNP** | Mtandao wa Jinsia Tanzania |
| **TICD** | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru |
| **UNFPA** | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu |
| **UZIKWASA** | Uzima Kwa Sanaa |
| **WMJJWM** | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |
| **WiLDAF** | Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika |

# SURA YA KWANZA

# MWONGOZO WA TAIFA WA UENDESHAJI MAJADILIANO KUHUSIANA NA MILA NA DESTURI ZENYE MADHARA KWA JAMII

## 1.1. Utangulizi

Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ni mojawapo ya ukiukwaji wa haki za binadamu ulioenea na kufanyika katika jamii nyingi na huvuka mipaka, rangi, matabaka, kabila na hata dini. Ukatili huu una madhara makubwa kiafya, kijamii na kiuchumi kwa mtu binafsi, familia yake na jamii kwa ujumla. Wanawake na watoto ambao ni waathirika wa vitendo vya ukatili, ikiwa ni pamoja na mila na desturi zenye kuleta madhara kama vile ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni mara nyingi hupata athari za muda mrefu za kihisia, matatizo ya kimwili, kiakili na kiafya na changamoto za afya ya uzazi salama. Pia, wapo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza. Aidha**,** madhara ya vitendo vya unyanyasaji kwa wanawake, watoto, familia na jamii kwa ujumla ni kikwazo kikubwa katika kupunguza umaskini ili kufikia usawa wa kijinsia na hatimaye kuleta mabadiliko chanya kwa kujenga jamii salama yenye amani bila vitendo vya unyanyasaji.

Matokeo ya utafiti uliofanyika mwaka 2009 na 2010 kuhusu Hali ya Ukatili dhidi ya Watoto pamoja na Utafiti wa Afya ya Uzazi na Watoto na Viashiria vya Malaria Tanzania wa mwaka 2015/16 unaonesha kuwa pamoja na jitihada za Kitaifa za kukabiliana na vitendo hivyo, lakini kuenea kwa ukatili dhidi ya

wanawake na watoto ikiwemo ukatili wa kijinsia, mimba na ndoa za utotoni na ukeketaji bado uko juu nchini. Aidha, masuala haya hukubalika katika jamii nyingi nchini Tanzania na kwa kiasi kikubwa huonekana kama ni suala la kaya, familia au jamii husika ambalo linashughulikiwa na kutatuliwa ndani ya mifumo ya jamii husika. Matokeo yake, viwango vya utoaji wa taarifa kwenye Mamlaka husika ikiwemo Jeshi la Polisi kuhusu masuala ya afya, ulinzi wa watoto au jamii vinaendelea kuwa vya chini na mateso kwa wahanga wa vitendo vya ukatili unaendelea ikilinganishwa na idadi ya kesi za mashambulizi zilizotolewa taarifa katika tafiti mbalimbali nchini Tanzania. Hali hii inapunguza uwezo wa wanawake, wasichana na wavulana kufurahia haki zao za msingi kama binadamu na uhuru wao kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) 2017/18 – 2021/22. Huu ni mfumo mpana na jumuishi ambao unaweka hatua za kipaumbele kwa nchi ili kufikia Dira yake ya Maendeleo ya mwaka 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 pamoja na shabaha za kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

## 1.2. Umuhimu wa Mwongozo

Kipaumbele cha msingi katika Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na

Watoto nchini (MTAKUWWA) ni kuwezesha na kusaidia wanawake na watoto ili kuzuia, kujilinda pamoja na kukabiliana na vitendo vya ukatili popote na wakati wowote vinapojitokeza au kuonekana ili kupunguza kuongezeka kwa ukatili wa kijinsia, mimba na ndoa za utotoni na ukeketaji ifikapo 2021/2022. Ili kufanikisha hili, Mpango unakuza na kuwezesha mikakati mbalimbali; mojawapo ni uendelezaji wa mila na desturi chanya ambazo huwezesha wanawake, na kusaidia mahusiano yasiyo ya kikatili, yenye heshima, yaliyo chanya na yenye kukuza usawa wa kijinsia kupitia ushirikishwaji jamii ikiwa ni pamoja na viongozi wenye ushawishi katika jamii, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, wanaume na wavulana katika uhamasishaji, utetezi, majadiliano ngazi ya jamii na matukio mengine ya kijamii.

Mbinu hii, ambayo inatokana na ushahidi wa kimataifa, imetumiwa sana na Serikali, Mashirika ya Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Kidini kama njia muafaka ya kushughulikia visababishi vya kukosekana kwa usawa wa kijinsia ili kuleta mabadiliko ya mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii. Hata hivyo, licha ya kuenea na kuendelea kwa matumizi ya mkakati huu, hakuna Mwongozo wa Kitaifa, ambao unaweza kusaidia kusimamia viwango vya muundo, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya majadiliano ngazi ya jamii. Hali hii inafanya kuwepo kwa

changamoto katika kufuatilia matumizi yake, kuthibitisha ubora na kutathmini ufanisi na athari zake katika kupunguza vitendo vya ukatili nchini.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeona umuhimu wa kuandaa Mwongozo utakaotumika kuandaa jukwaa kwa ajili ya jamii kupata fursa ya kujadiliana kwa tija kuhusu kuwepo kwa mila na desturi zenye manufaa ili ziendelezwe na kutokomeza zile zenye kusababisha madhara na kuendekeza uhusiano usio  na usawa. Hivyo, Mwongozo unahimiza jamii kujitolea katika kuibua, kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja na kupendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya wale wote wanaoendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

### 1.3. Lengo Kuu

Kukuza na kuimarisha mila na desturi chanya zinazowezesha jamii kujenga mahusiano mazuri yenye kuleta heshima na yanayozingatia usawa wa kijinsia pamoja na kulinda Haki za wanawake na watoto dhidi ya aina zote za vitendo vya ukatili ndani ya jamii.

### 1.4. Malengo Mahsusi

i. Kutambua na kuendeleza mila na desturi chanya zinazoimarisha usawa wa kijinsia katika jamii;

ii. Kusaidia jamii kutambua na kukabiliana na mila na desturi zinazoendeleza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
iii. Kuiwezesha jamii kufikia muafaka na kuweka mikakati ya pamoja ya kutokomeza mila na desturi zenye kuleta madhara;
iv. Kukuza na kuiwezesha jamii kuibua na kutekeleza mbinu shirikishi za kutokomeza vitendo vya ukatili; na
v. Kuandaa jukwaa kwa ajili ya kuwezesha makundi maalum hususan wanawake na watoto kupaza sauti zao.

### 1.5. Watumiaji wa Mwongozo wa Uendeshaji Majadiliano Ngazi ya Jamii

Walengwa wa Mwongozo huu ni pamoja na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, Asasi za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Kidini na Kijamii ambayo hupanga na kuendesha majadiliano hayo ngazi ya jamii ili kushughulikia changamoto hizi pamoja na kuimarisha uwezo wa jamii katika kuendeleza mila na desturi nzuri na kukabiliana na zile ambazo zinachochea na kuendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Wadau wote wanaoendesha majadiliano ngazi ya jamii wanawajibika kuhakikisha kuwa kuna uzingatiaji wa Mwongozo huu wakati wa kuandaa na kutekeleza majadiliano hayo. Katika utekelezaji halisi, watekelezaji kutoka Sekta Binafsi watapaswa

kufanya kazi chini ya uongozi wa Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI). Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya nchini zitatoa mwongozo unaohitajika wakati wa Utekelezaji. Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Wilaya ndio watakuwa wasimamizi na waangalizi wa shughuli za majadiliano ngazi ya jamii katika majukumu yao ya kila siku. Watekelezaji kutoka Sekta Binafsi wataweza kufika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa kwa ajili ya majadiliano ngazi ya jamii kupitia mwongozo kutoka kwa Maafisa hao wa Serikali.

Mwongozo huu unapaswa kusomwa kikamilifu kabla ya kuendesha vipindi vya majadiliano ngazi ya jamii.

### 1.6. Majukumu na Wajibu wa Wadau

Yafuatayo ni majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa Mwongozo huu:

#### 1.6.1. Ngazi ya Wizara

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WMJJWM) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Majadiliano ngazi ya Jamii inayowiana na mfumo na taratibu za Serikali kwa kuzingatia yafuatayo:

i. Kuhakikisha kuwa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi Zenye Madhara Kwa Jamii unaingizwa kwa ufanisi katika mipango na mikakati ya Serikali katika ngazi mbalimbali;
ii. Kutoa mwongozo wa kisera katika uratibu na utekelezaji wa jumla wa Mwongozo wa Kitaifa wa kuendesha majadiliano ngazi ya jamii yenye ufanisi;
iii. Kusambaza Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi Zenye Madhara Kwa Jamii;
iv. Kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji wenye ufanisi wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara Kwa Jamii unaoendana na mahitaji;
v. Kuhakikisha utoaji wa taarifa za majadiliano ngazi ya jamii unazingatia viwango vilivyotolewa na Mwongozo huu;
vi. Kufanya mapitio ya taarifa za maendeleo ya Mikoa na kushauri ipasavyo; na
vii. Kufanya mapitio na kuhuisha Mwongozo huu pale inapobidi.

### 1.6.2. Ngazi ya Mkoa

Sekretarieti ya Mkoa inawajibika kwa shughuli zote zinazojumuisha usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa majadiliano ngazi ya jamii kwa:

i. Kuhakikisha kwamba Halmashauri zote na washirika au wadau wanaotekeleza

Mwongozo huu wanatekeleza afua zote muhimu;

ii. Kutoa msaada wa kiufundi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji bora na wenye ufanisi wa Mwongozo huu;

iii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii katika Halmashauri zote nchini; na

iv. Kuunganisha taarifa za maendeleo za Kikanda kwenye majadiliano ngazi ya jamii na kuziwasilisha katika ngazi husika.

### 1.6.3. Ngazi ya Halmashauri

Ngazi ya Halmashauri inawajibika kutekeleza shughuli zote zinazojumuisha usimamizi na uratibu wa majadilianao ngazi ya jamii kwa kufanya yafuatayo:

i. Kuhakikisha kuwa bajeti inatengwa kwa ajili ya usambazaji, uelekezaji na utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii;

ii. Kuwapitisha na kuwaelekeza viongozi wa Halmashauri na wadau wengine muhimu kuhusu Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii;

iii. Kusaidia kuwajengea uwezo Wawezeshaji wa majadiliano ngazi ya jamii kwenye Halmashauri;
iv. Kuwezesha usimamizi wa pamoja wa utekelezaji wa Mwongozo wa Majadiliano kuhusiana na Mila na Desturi Zenye Madhara kwenye Jamii;
v. Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii katika Kata na Vijiji/Mitaa; na
vi. Kuunganisha taarifa za maendeleo za Halmashauri kwenye majadailiano ngazi ya jamii na kuziwasilisha katika ngazi husika.

#### 1.6.4. Ngazi ya Kata/Kijiji/Mtaa

Ngazi ya Kata/Kijiji/Mtaa inawajibika kwa shughuli zote zinazojumuisha utekelezaji, usimamizi, na uratibu wa utekelezaji wa majadiliano ngazi ya jamii kwa kufanya yafuatayo:

i. Kubainisha maeneo yenye hatari kubwa katika utekelezaji wa afua za kukabiliana na mila na desturi zenye kuleta madhara kwa kuandaa mikakati/mipango ya kuendesha majadiliano ngazi ya jamii;
ii. Kuwezesha matumizi ya Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii;

iii. Kuandaa ramani ya huduma saidizi zinazopatikana kwa wahanga na waathirika wa vitendo vya ukatili;
iv. Kusimamia na kuhakikisha kuwa kuna uzingatiaji Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii miongoni mwa wadau wote wanaoutekeleza; na
v. Kutayarisha taarifa za maendeleo ya majadiliano ngazi ya jamii ili kupata fursa ya kubadilishana uzoefu na Mamlaka zingine muhimu.

### 1.6.5. Wadau

Wadau wanawajibika kusaidia utekelezaji wa Mwongozo katika ngazi mbalimbali kwa kufanya yafuatayo:

i. Kushirikiana na OR-TAMISEMI na WMJJWM kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii kitaalam na kifedha;
ii. Kushirikiana na Serikali kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo; na
iii. Kushirikiana na WMJJWM kuchapisha, kusambaza nakala za Mwongozo na kufanya mapitio pale inapohitajika.

### 1.6.6. Jamii

Jamii inawajibika kwa shughuli zote zinazojumuisha utekelezaji wa Mwongozo kwa kufanya yafuatayo:

i. Kubaini mila na desturi nzuri katika jamii na kuweka mikakati/mipango ya kuziendeleza;
ii. Kubaini mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii na kupanga mikakati/mipango ya kuzitokomeza ili kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
iii. Kutoa taarifa za kesi za vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto zinazotokea ndani ya jamii;
iv. Kuhamasishana, kuelimishana na kuchukua hatua stahiki ya kushughulikia athari za ukatili pamoja na kutoa msaada wa awali kwa waathirika;
v. Kushirikiana na wadau wanaoendesha majadiliano ngazi ya jamii ili kuwezesha utekelezaji wenye ufanisi;
vi. Kushirikiana na Serikali pamoja na wadau kutafuta rasilimali za kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo; na
vii. Kutunza kumbukumbu za matukio, jitihada na hatua zilizochukuliwa za kutokomeza mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii kupitia mabalozi wa mabadiliko chanya ya tabia.

### 1.7. Mpangilio wa Mwongozo

Mwongozo wa Taifa wa Uendeshaji Majadiliano Kuhusiana na Mila na Desturi zenye Madhara kwa Jamii umegawanyika katika sura tano. Sura ya Kwanza inaelezea utangulizi kuhusu Mwongozo huu pamoja na malengo mahsusi. Sura ya Pili inatoa maelezo ya kina kuhusu Majadiliano ya Kijamii. Sura ya Tatu inahusu Mwongozo kwa Wawezeshaji ambapo mbinu na kanuni mbalimbali za uwezeshaji zimefafanuliwa. Aidha, Sura ya Nne inatoa maelezo kuhusu Kupanga na Kuendesha Majadiliano yenye Ufanisi Ngazi ya Jamii na Sura ya Tano inaangazia Utunzaji wa Kumbukumbu, Ufuatiliaji na Tathmini. Mwishoni mwa Mwongozo huu kuna viambatisho vyenye mada mbalimbali muhimu za kufundisha.

# SURA YA PILI

# MAJADILIANO YA KIJAMII

Majadiliano ya kijamii ni jukwaa la kuwezesha ushiriki wa jamii, wakiwemo wazazi, vijana na viongozi wa jamii katika majadiliano ya pamoja kuhusu usawa wa kijinsia, ukatili dhidi ya wanawake na watoto juu ya mila na desturi zenye kuleta madhara. Mila na desturi hizo ni pamoja na; ukeketaji, kurithi na kutakasa wajane, mimba na ndoa za utotoni, na masuala yanayohusu haki za wanawake ikiwemo umiliki wa ardhi, urithi wa mali zinazohamishika na zisizohamishika.

## 2.1. Majadiliano Ngazi ya Jamii ni Nini?

Majadiliano ngazi ya jamii ni mchakato wa utambuzi wa pamoja wa tatizo na uchambuzi unaopelekea kurekebisha na kuelekeza upya jamii na wadau kuchukua hatua stahiki ili kufikia mustakabali unaokubalika na wote. Ni mchakato shirikishi wa kubadilishana taarifa kati ya watu au makundi ya watu kwa lengo la kufikia maelewano na maazimio ya pamoja.

Majadiliano yenye ufanisi huwezesha jamii kujenga uwezo wa kutambua masuala yanayohusiana na mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii, huimarisha uelewa wao juu ya sababu za msingi za kuwepo kwa mila na desturi hizo, na kupendekeza jinsi ya kuchukua hatua madhubuti kubadilisha mitazamo yao kwa lengo la kuboresha maendeleo

na ustawi wa wanawake na watoto. Mbinu hiyo inahimiza jamii kuwajibika kwa kile kinachotokea katika jamii yao badala ya kunyosheana vidole; hivyo kufikia makubaliano yakinifu katika kutatua changamoto zao. Majadiliano haya hukuza moyo wa umoja ndani ya jamii kwa kufanya kazi pamoja kutafuta suluhu yenye kuleta tija kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, kijamii au kiafya.

Majadiliano ngazi ya jamii huwezesha jamii kuandaa maazimio kwa ajili ya hatua mbalimbali za utekelezaji.

### 2.2. Manufaa ya Majadiliano

Majadiliano ngazi ya jamii yenye ufanisi yanayowezesha jamii kuazimia na kuchukua hatua dhidi ya changamoto, masuala na upungufu uliotambuliwa kwa njia shirikishi yanalenga:

i. Kutangaza jukwaa ili wasiosikika wapaze sauti zao wasikike;
ii. Kukuza mawasiliano na mahusiano ya kijamii kati ya makundi yenye mitazamo tofauti katika jamii;
iii. Kuwezesha jamii kuwa na uelewa wa kina juu ya hali, desturi, maslahi, changamoto pamoja na kupendekeza mikakati kabambe ya kushughulikia mabadiliko ya tabia;
iv. Kujenga uwezo wa rasilimali watu wenye ustadi wa kuongoza na kuleta mabadiliko chanya katika jamii;

v. Kuwezesha utambuzi wa watu na wadau muhimu katika jamii ili kuimarisha mawasiliano na ubia endelevu wa kutatua changamoto za kijamii;
vi. Kukuza uwajibikaji na kuchochea utayari wa jamii kuchukua hatua za kutekeleza afua zinazokubalika kutatua changamoto za kijamii; na
vii. Kuwezesha ushiriki wa jamii ili kuwa na utayari wa kujitolea katika kutatua changamoto za kijamii kwa ajili ya kudumisha mabadiliko ya tabia.

## 2.3. Malengo ya Majadiliano Ngazi ya Jamii

i. Kutambua na kukuza mila na desturi chanya ambazo zinazowezesha jamii kuimarisha uhusiano usio na ukatili, wenye heshima na unaozingatia usawa wa kijinsia;
ii. Kuhamasisha jamii juu ya faida za kuachana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi kwa waathirika wa ukatili;
iii. Kuwezesha majadiliano juu ya mila na desturi zinazoathiri usawa wa kijinsia na ustawi wa wanawake, wasichana, wanaume, wavulana na watoto ili kuweka mikakati ya kutokomeza vitendo vya ukatili ndani ya jamii; na

iv. Kuhamasisha jamii kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

**2.4. Changamoto za Majadiliano Ngazi ya Jamii**

i. Kuandaa na kuendesha majadiliano ngazi ya jamii hutumia muda mwingi. Hivyo, inahitaji uvumilivu, ustadi na mbinu za uwezeshaji pamoja na ukumbi wenye utulivu ili washiriki wapate fursa ya kushiriki kikamilifu;
ii. Maandalizi duni ya mipango yanaweza kuathiri ubora wa majadiliano ngazi ya jamii;
iii. Wale wanaopinga maendeleo ya kijamii wanaweza kukataa kushiriki katika majadiliano.
iv. Uwezekano wa kupata ushiriki hafifu wa walengwa (idadi ndogo ya washiriki) kutokana na mwiingiliano wa kalenda za matukio au shughuli za kiuchumi na kijamii hasa sherehe za kijadi, kipindi cha kilimo au mavuno; na
v. Mila na desturi ya uzingatiaji wa umri na jinsi wakati wa uwezeshaji wa majadiliano ya kijamii huweza kuathiri ushiriki au mchango wa kijamii, kwa mfano, kundi la wazee kuwezeshwa na mtu ambaye si wa makamo au mzee kama wao.

## 2.5. Kanuni Muhimu

### 2.5.1. Umuhimu wa Kuwa Makini katika Masuala ya Kijinsia

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia (2001), *"Jinsia ni suala muhimu katika ufanisi wa maendeleo, sio tu suala la usahihi wa kisiasa au wema kwa wanawake. Ushahidi unaonesha kwamba wanaume na wanawake wanapokuwa sawa, uchumi huelekea kukua kwa kasi, umaskini hupungua kwa kiwango kikubwa na ustawi wa wanaume, wanawake na watoto huimarishwa."*

Mbinu zinazozingatia masuala ya usawa wa kijinsia wakati wa majadiliano ngazi ya jamii huwa na manufaa kwa washiriki pamoja na jamii husika kwa ujumla. Mbinu hizo zinamwezesha mwezeshaji kuweka mazingira bora na rafiki ya kujifunzia yenye usawa na endelevu kwa wote. Kwa hiyo, ni jukumu la mwezeshaji kuhakikisha washiriki wanakuwa huru kutoa mawazo yao wakati wa majadiliano kupitia mbinu shirikishi za uwezeshaji ikiwemo kuuliza maswali.

### 2.5.2. Kulinda na Kuepusha Madhara

Mwezeshaji anatakiwa kuwa makini wakati wa kuwasilisha mada zinazohusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto, mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii ili kukubalika na jamii husika. Kanuni kuu ya Mwongozo huu ni usidhuru (*Do No Harm*). Hii ina maana kwamba majadiliano ngazi ya

jamii hayapaswi kuhatarisha amani na usalama kwa washiriki na jamii kwa ujumla.

# SURA YA TATU

# MWONGOZO KWA WAWEZESHAJI

## 3.1. Mbinu za Uwezeshaji

Majadiliano ngazi ya Jamii yanatarajiwa kuwa jukwaa ambalo washiriki wataweza kushiriki kwa uhuru katika kutoa maoni yao juu ya kile kinachoendelea ndani ya jamii bila hofu ya unyanyapaa, ubaguzi au aibu kutoka kwa washiriki wengine. Utayari wa washiriki kutoa mawazo yao hutegemea ujuzi na mbinu za mwezeshaji. Mwezeshaji anapaswa kuwa na ujuzi wa kuwawezesha washiriki wa majadiliano kujisikia huru na salama kimwili na kihisia. Mwezeshaji pia anapaswa kuwa na ujuzi wa kuhimiza washiriki wa majadiliano ngazi ya jamii kutambua mila na desturi ili kuweka mikakati maalum ya kukabiliana na zenye kuleta madhara katika jamii.

Mbinu ambazo mwezeshaji anazopaswa kuzitumia ili kuwezesha washiriki kuchangia au kutoa mawazo yao ni pamoja na:-

i. Subira;
ii. Umakini katika masuala muhimu;
iii. Huruma;
iv. Kujitambua;
v. Stadi na umakini wa kusikiliza;

vi. Maarifa na uwezo wa kuongoza majadiliano shirikishi;
vii. Uwezo wa kushirikisha na kuwezesha utatuzi wa migogoro;
viii. Ujuzi na uwezo wa kuwasiliana na washiriki kwa kutumia lugha rahisi na inayoeleweka; na
ix. Utunzaji wa muda.

### 3.2. Mbinu za Ujifunzaji kwa Watu Wazima

Ni muhimu kuzingatia kuwa, watu wazima wanaojifunza wana uzoefu wa miaka mingi na wana uelewa wa mambo mengi. Pia watu wazima wana uelewa mpana wa masuala ya maadili, imani, mila na desturi mbalimbali katika jamii ambapo hujifunza kwa kuhusianisha maarifa na habari mpya na uzoefu walionao. Katika hali kama hiyo, mara nyingi hupenda kutumia ujuzi na uzoefu walionao kutatua changamoto zilizopo katika jamii. Kwa hiyo, wakati wa kuwawezesha, mwezeshaji anapaswa kuwa na umakini wa hali juu ili kutumia ujuzi na uzoefu wao kikamilifu kutatua changamoto zilizopo.

Mwezeshaji hana budi kuheshimu tofauti za kiimani, kidini, kimila na desturi za washiriki na kuwawezesha washiriki kujua kwamba wana haki kuhusiana na maadili, imani na maoni yao, na si lazima kila mtu kushiriki katika imani ya mwingine.

Aidha, ni muhimu kwa mwezeshaji kutumia mbinu mbalimbali kuchangamsha washiriki kila inapowezekana ikiwemo mapumziko ya mara kwa mara, hata kama ni ya dakika 2 za kujinyoosha. Vilevile, maswali na maoni ya kila mshiriki yaheshimiwe na kufanyiwa kazi. Mwezeshaji aepuke kusema, "tumeshughulikia hilo" pale mtu anapouliza swali linalojirudia. Kama mwezeshaji, huhitaji kuwa na majibu yote, cha msingi ni kujua pa kwenda au nani wa kumpigia simu, ili kupata majibu au ufafanuzi wa suala husika.

### 3.3. Stadi Shirikishi za Kujifunza

Mafunzo shirikishi ni mbinu inayohusisha mwezeshaji ambaye huwaongoza na kuwahimiza washiriki kuwajibika ipasavyo katika mchakato wao wa kujifunza. Kwenye mbinu hii, mwezeshaji huzungumza machache zaidi huku washiriki wakitumia uzoefu walionao kutatua changamoto zao kwa pamoja. Mbinu hii imedhihirika kuwa ya manufaa sana wakati wa kufanya kazi na washiriki watu wazima ambao huenda hawakuzoea kuwa wanafunzi. Mbali na hayo, mbinu shirikishi ya kujifunza inachukuliwa kuwa mbinu muafaka ya kukuza mabadiliko ya kijamii kupitia kuhamasisha mageuzi ya msingi katika miundombinu mbalimbali ya kijamii.

### 3.4. Miiko na Maadili ya Mwezeshaji

Mwezeshaji anapoongoza vipindi vya majadiliano katika jamii anatarajiwa kuzingatia miiko na maadili kama inavyoonesha hapa chini:

| Na. | Miiko na Maadili | Vidokezo vya Ufafanuzi |
|---|---|---|
| 1. | Kuheshimu, kukuza na kulinda haki za binadamu | Wawezeshaji wanapaswa kufahamu haki za kijinsia na kiafya na haki nyingine za wanajamii kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi. |
| 2. | Onyesha umakini katika masuala ya kitamaduni | Mwezeshaji ajue utamaduni wa jamii husika wakati wa kuwezesha majadiliano yanayoendelea hasa umakini katika kushughulikia masuala ambayo kuna kutokukubaliana.<br><br>Wawezeshaji wanapaswa kufahamu kwamba, kuwa makini kuhusu mila na imani za jamii husika haimaanishi kukubaliana na mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii ikiwemo ukeketaji, |

| Na. | Miiko na Maadili | Vidokezo vya Ufafanuzi |
|---|---|---|
| | | ndoa za utotoni, ukatili wa kijinsia, n.k. |
| 3. | Heshimu utofauti | Wawezeshaji wanapaswa kuheshimu tofauti za washiriki kwa misingi ya tamaduni, kabila, rangi, lugha, ulemavu, muktadha wa kijamii na kiuchumi, makazi, n.k.<br><br>Hakikisha kwamba shughuli za majadiliano ngazi ya jamii zinakidhi mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii (mahali pa kuendeshea vipindi vya majadiliano, lugha inayotumika, eneo la kufanyia majadiliano, n.k.). |
| 4. | Kukuza usawa wa kijinsia na fursa sawa | Sisitiza umuhimu wa usawa wa kijinsia na fursa sawa kwa wote katika hatua zote za uendeshaji |

| Na. | Miiko na Maadili | Vidokezo vya Ufafanuzi |
|---|---|---|
| | kwa wote. | wa majadiliano ngazi ya jamii. |
| 5. | Kuhakikisha na zingatia usiri | Hakikisha usiri unazingatiwa wakati wote wa majadiliano ngazi ya jamii. Wawezeshaji wote wanapaswa kuwa na ufahamu juu ya jinsi ya kulinda usiri wa wale wanaoshiriki katika majadiliano ngazi ya jamii. |
| 6. | Usilazimishe maadili, wezesha kujitathmini kwa kuzingatia maadili | Wawezeshaji wanapaswa kuwa na ujuzi wa kuzingatia maadili yao na kuheshimu maadili ya watu wengine wakati wa majadiliano ngazi ya jamii.<br><br>Wawezeshaji hawapaswi kulazimisha washiriki kufuata maadili yao wakati wa majadiliano. |
| 7. | Epuka kujiwakilisha vibaya, zingatia mipaka ya kufichua taarifa | Wawezeshaji wanapaswa kujibu maswali kwa uaminifu kuhusu tabia zao na kuelewa kwamba hawalazimishwi kushirikisha jamii zaidi ya kile kinachokubalika. |

| Na. | Miiko na Maadili | Vidokezo vya Ufafanuzi |
|---|---|---|
| | binafsi | |
| 8. | Toa taarifa iliyohuishwa, sahihi na isiyo na upendeleo. | Wawezeshaji wanapaswa kuwa na taarifa zilizohuishwa na sahihi ili kuwawezesha kuwasilisha taarifa zilizo sahihi na zisizo na upendeleo wakati wa majadiliano ngazi ya jamii.<br><br>Weka mazingira rafiki ambayo ujifunzaji endelevu unaweza kufanyika na hakikisha unatoa nyenzo muhimu kwa ajili ya rejea. |
| 9. | Epuka kutumia vibaya nafasi yako kama Mwezeshaji | Wawezeshaji wanapaswa kuwa na mbinu na ujuzi unaowawezesha kuwajibika na kutumia nafasi zao vizuri. |

## Vidokezo Vingine: Fanya na Usifanye za Mwezeshaji

| FANYA (DO's) | USIFANYE (DON'Ts) |
|---|---|
| • Fanya maandalizi mapema.<br>• Hakikisha kwamba lengo la kipindi limefafanuliwa kwa uwazi na kwa kina na pia nyenzo za kujifunzia zimesambazwa kwa washiriki kabla au wakati wa majadiliano.<br>• Epuka tabia zinazotatiza na kushusha hadhi ya washiriki kifikra.<br>• Tumia zana za kufundishia na ziweke ambapo kila mtu aweze kuziona.<br>• Ongea kwa uwazi na kwa sauti ya kutosha.<br>• Tumia mtiririko wa kimantiki unaounganisha mada moja na nyingine.<br>• Andika maandishi rahisi | • Usizungumze na chati mgeuzo (*flipchart*), ubao au skrini.<br>• Usizibe zana au vielelezo vya kufundishia.<br>• Usisimame sehemu moja, zunguka chumba.<br>• Usifikirie kuwa kila mtu anaweza kusoma na kuelewa kwa kiwango sawa.<br>• Usisome moja kwa moja kutoka kwenye Mwongozo wakati wa |

| FANYA (DO's) | USIFANYE (DON'Ts) |
|---|---|
| na kwa kukoleza.<br>• Toa maelekezo yanayoeleweka.<br>• Hakiki iwapo maelekezo yako yameeleweka.<br>• Zingatia mawasiliano ya ana kwa ana na washiriki.<br>• Fahamu mawasiliano ya lugha ya mwili ya washiriki wako.<br>• Zingatia majadiliano chanya yenye kujenga kulingana na suala linalojadiliwa.<br>• Himiza maoni na maswali kutoka kwa washiriki wote.<br>• Sikiliza.<br>• Toa mrejesho.<br>• Fanya muhtasari na inapobidi kwa kufafanua kile ambacho kimesemwa hivi karibuni na kuangalia usahihi.<br>• Tumia muda vizuri.<br>• Kuwa tayari | kuwasilisha mada kwenye kipindi.<br>• Usipuuzie maoni na mrejesho wa washiriki.<br>• Usiwafokee washiriki |

| FANYA (DO’s) | USIFANYE (DON’Ts) |
|---|---|
| kunyumbulika na mvumilivu. | |

### 3.5. Mbinu za Uwezeshaji Zilizochaguliwa

Mwezeshaji hana budi kuwa na ujuzi katika kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji wa jamii kujadili na kufikia muafaka, ambao huchochea mabadiliko chanya ya tabia ili kuchukua hatua katika kuimarisha mahusiano ya kijamii. Baadhi ya mbinu zilizochaguliwa zimefafanuliwa kwa ufupi hapa chini kwa ajili ya rejea.

#### 3.5.1. Mbinu ya Kujifunzia Kuzingatia Kiini cha Tatizo

Hii ni mbinu ya kisaikolojia na kijamii ambayo inasimamia mchakato wa elimu ya watu wazima ambayo inazingatia kiini cha tatizo. Mbinu hii huwezesha kuweka mikakati ya kutatua tatizo baada ya kuligundua kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

| **Jamii - Kiini** (Kuandaa Mazingira) | **Ibua Tatizo** (Pa Kuanzia) | **Kujitambua** (Uchambuzi) | **Hatua za Utatuzi** (Suluhisho) |
|---|---|---|---|
| Jenga uhusiano mzuri kwa kusalimian | 1. Ulisikia au kuona nini? | 3. Je, hii hutokea katika jamii | 5. Je, tunaweza kufanya nini kuhusu hilo? |

| **Jamii - Kiini** (Kuandaa Mazingira) | **Ibua Tatizo** (Pa Kuanzia) | **Kujitambua** (Uchambuzi) | **Hatua za Utatuzi** (Suluhisho) |
|---|---|---|---|
| a na washiriki na kutaja majina yao. Kukuza usawa kwa kukaa kwenye duara na washiriki, kutazamana ana kwa ana na tumia uzoefu wao kujifunza<br><br>Tofautisha mbinu za kufundishia na kuchanga msha darasa. | | yetu?<br><br>Toa mifano | Nini?<br><br>Lini?<br><br>Wapi?<br><br>Vipi?<br><br>Nani? |
| | 2. Ni nini kilikuwa kikiendelea? au Tatizo kuu lilikuwa nini na kwa nini? | 4. Kwa nini hii hutokea (sababu)? | |

Mbinu hii ya kujifunza inasisitiza yafuatayo:-

1. Mazingira rafiki ya kujifunzia hayana budi kuandaliwa ili kuvutia washiriki na kuwafanya wajisikie vizuri wanapojifunza;

2. MWANZO inaweza kuwa ni picha, hadithi, wimbo, n.k., inaonesha tatizo rahisi na linaloweza kutatulika, ambalo linalenga kuhimiza majadiliano miongoni mwa washiriki;

3. Hatua ya tatu inaongoza kutoka kwa mwanzilishi hadi hali halisi ya maisha na kuiwezesha jamii kutoa mifano kutokana na uzoefu wao wenyewe kwenye jamii; na

4. Hatua ya nne ya kujifunza kwa mafanikio ina mwelekeo wa vitendo na inapaswa kuwaongoza washiriki katika mpango wa utekelezaji kuhusu jinsi watakavyoshirikiana kutatua tatizo walilonalo. Makubaliano haya yanaweza kuwa mpango wa utekelezaji wa pamoja au tamko lililotolewa na washiriki wote.

### 3.5.2. Majadiliano ya Wazi

Haya ni majadiliano ambayo mshiriki huchangia kwa uhuru na uwazi maoni yake. Ni muhimu kujua kwamba, washiriki wote wako katika viwango sawa

vya kubadilishana mawazo na uzoefu. Hakuna mshiriki anayepaswa kuonekana kuwa na uelewa mdogo au mkubwa kuliko wengine. Mawazo yote ni ya thamani, ingawa ni baadhi tu yanaweza kuwa muhimu. Wote wako huru kukosoa au kuunga mkono wazo wakiwa na sababu maalum za kufanya hivyo.

### 3.5.3. Majadiliano ya Kikundi

Majadiliano ya kikundi kidogo cha watu 3 hadi 10 ni mbinu muafaka inayowahimiza washiriki kuchambua, kuunganisha athari za mila na desturi fulani ndani ya jamii na kutathmini maarifa wanayopata. Majadiliano ya kikundi yanaweza kuongozwa na mwezeshaji au washiriki wenyewe.

### 3.5.4. Majadiliano ya Kikundi Lengwa

Washiriki wanaweza kujadili katika vikundi vidogo vya watu 8 hadi 12 juu ya somo au kazi waliyopewa kwa kusimamiwa na mwezeshaji. Kazi ya kuwaweka washiriki katika vikundi inafanywa kulingana na vigezo vilivyochaguliwa na mwezeshaji kama vile eneo la kijiografia, shughuli za kiuchumi, elimu, umri, jinsi (jinsi moja au mchanganyiko), ulemavu au kulingana na taarifa inayohitajika. Kuwa katika kikundi huwezesha uelewa wa kina wa kazi unaotakiwa kuitikiwa kwa sababu wanakikundi huanza kwa kujadili kile

wanachohitaji kujibu, kisha washiriki huchangia maoni yao kwa uhuru zaidi. Hata hivyo, kikundi lengwa kikiwa ni kikubwa sana husababisha kupungua kwa ufanisi wa uchangiaji.

### 3.5.5. Igizo

Inajumuisha tamthilia fupi fupi (kama dakika 5 hadi 10) zinazotumiwa kuelezea pointi au hali halisi. Igizo linaweza kutumika kwa mfano katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Ni muhimu kwa waigizaji kutoa ufafanuzi wa kutokuwa na uhalisia katika nafasi walizoigiza baada ya kumalizika kwa igizo hususan pale ambapo wameigiza kwenye nafasi zenye sifa mbaya au zisizokubalika. Lengo ni kuepusha waigizaji kupewa sifa ya kudumu ya wahusika waliouvaa wakati wa tamthilia. Mbinu hii inafaa kwa ajili ya kuchambua tabia au mitazamo fulani ndani ya jamii kwa lengo la kulibadilisha.

### 3.5.6. Bungua Bongo

Ni mbinu inayohusisha washiriki wote katika uchangiaji wa mawazo juu ya mada husika. Inatumika kutoa suluhisho mbadala kwa tatizo linalowakabili washiriki wanaowakilisha jamii yenye mitazamo na asili tofauti. Njia hii inasaidia kuhimiza washiriki wote wa kikundi kuzungumza na kuibua njia bunifu iliyobora na kamili kutoka kwa wanakikundi wote kwa pamoja. Wakati wa shughuli

ya kubungua bongo na kujadiliana, mwezeshaji anatarajiwa kukubali na kuandika mawazo yote bila kuhariri na kuchambua majibu ya washiriki.

### 3.5.7. Kisa Mkasa

Hii inahusisha uwasilishaji wa kisa mkasa kwa washiriki ikifuatiwa na majadiliano kuhusu kisa hicho. Visa mkasa ni simulizi ya matukio halisi au ya kufikirika inayohusiana na mada zinazojadiliwa katika jamii. Mwezeshaji huwasilisha kisa mkasa ambacho huweza kujadiliwa na kundi zima au katika vikundi vidogo.

### 3.5.8. Mti wa Matatizo na Suluhisho

Hizi zinajumuisha seti za matatizo au suluhisho za visababishi vikuu vinavyohusiana na matatizo. Kila sababu ya tatizo au suluhisho ina mizizi ambayo hatimaye hujenga mahusiano sawa na muundo wa mti. Mti unaweza kupinduliwa chini juu ili mizizi iwe matawi. Kwa njia hii suluhisho pana linaweza kugawanywa katika suluhisho ndogo ndogo.

Miti ya matatizo na suluhisho ni michoro na zana za taswira za kujadili malengo mapana, ambayo hugawanywa zaidi katika malengo na shughuli. Yanaweza kuwa muhimu kwa ajili ya kuchambua matokeo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu yanayotarajiwa na athari zake.

### 3.5.9. Bakuli la Jinsia

Njia hii inafanya kazi na kundi la washiriki wa jinsia mchanganyiko. Kwa kawaida duara mbili (duara la ndani na duara la nje) huandaliwa. Wanawake huketi kwenye duara la ndani huku wanaume wakiwa kwenye duara la nje. Wanawake wakiwa wamekaa kwenye duara la ndani wanaambiwa kujadili masuala yanayowaathiri kwa kutumia maswali yaliyotayarishwa kwa ajili yao. Kwa wakati huu, wanaume hawaruhusiwi kutoa maoni kwa njia yoyote ile. Kisha wanaume pia huketi kwenye duara la ndani huku wanawake wakielekea kwenye duara la nje. Utaratibu huo huo hurudiwa kwa wanaume bila kuruhusu wanawake kutoa maoni yao.

Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, katika baadhi ya jamii (hususan wanaume na wake zao wanapohudhuria kikao), inaweza kuwa vigumu kwa wanawake kujieleza kwa uhuru na uwazi kwa sababu wanaogopa kuzungumza hadharani mbele ya waume zao. Hivyo, ni bora kuwahimiza kuzungumza kwa ujumla wakati wa kushiriki.

### 3.5.10. Shughuli za Jinsi Moja

Shughuli hii inatenganisha wanaume na wanawake ili kuchunguza suala fulani tofauti kwa mtazamo wao na kisha kutoa taarifa kwenye kundi kubwa la jinsi zote mbili. Shughuli hizi za jinsi moja

zinapaswa kuongozwa na wawezeshaji wa jinsi moja na kutoa fursa kwa washiriki kuwasiliana bila kikwazo kutoka kwa wenzi wao na huunganishwa na washiriki wengine wa jinsi moja. Shughuli hizi huwapa wawezeshaji maarifa ya kina kutoka kwa washiriki binafsi na kuleta mabadiliko katika mchakato na hatimaye kuifanya programu kuvutia zaidi.

# SURA YA NNE

# KUPANGA NA KUENDESHA MAJADILIANO YENYE UFANISI NGAZI YA JAMII

Maandalizi ya majadiliano yenye ufanisi ngazi ya jamii na utekelezaji wake yanahitaji maandalizi mazuri ili vipindi hivyo vifanikiwe. Yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa na mwezeshaji wakati wa kupanga majadiliano yenye ufanisi ngazi ya jamii.

## 4.1. Kupanga Majadiliano Ngazi ya Jamii

### 4.1.1. Itifaki za Kuzingatia Kabla ya Majadiliano

Itifaki zote muhimu zinazohitajika kabla ya kufanya majadiliano zinapaswa kuzingatiwa na mwezeshaji wakati wa kuandaa majadiliano ngazi ya jamii. Hii ni pamoja na kupata ruhusa kutoka kwa mamlaka husika. Uongozi wa eneo linalokusudiwa la kijiografia unapaswa kufahamishwa kupitia mawasiliano rasmi.

### 4.1.2. Walengwa

Mwongozo huu unalenga kuleta mabadiliko chanya kwa watu wenye ushawishi kwenye jamii, waendelezaji wa vitendo vya ukatili, waathirika wa ukatili na wale walio katika hatari ya kufanyiwa ukatili hus.usan wanawake na watoto. Wakati wa kuzingatia hadhira lengwa kwa ajili ya majadiliano ngazi ya jamii, inashauriwa kwanza kuzingatia kama mada na mbinu zilizochaguliwa zinafaa kwa

mtazamo wa jinsi mchanganyiko au ni bora kutenganisha jinsi hizo mbili.

Uchaguzi wa washiriki kwa ajili ya majadiliano ngazi ya jamii unapaswa kuzingatia vikundi tofauti vya kijamii. Miundo ya kijamii inayopewa kipaumbele ni ile inayochukuliwa kuwa walezi na waendelezaji wa mila na desturi katika jamii kama vile viongozi wa kidini, wazee/viongozi wa jamii, wanaume na wavulana, pamoja na vikundi vya wanawake.

Ili kuhakikisha kwamba kila mtu anasikilizwa wakati wa majadiliano, idadi ya washiriki haipaswi kuzidi watu 25-30 kutegemeana na mpangilio wa majadiliano. Idadi ya watu ikizidi 30, itamuwia vigumu mwezeshaji kuhakikisha ushiriki wa kila mtu katika majadiliano. Hii inategemea kiwango cha umuhimu wa mada, muundo wa majadiliano na muda wake.

Viongozi wa jamii, wakiongozwa na mwezeshaji, wataongoza uteuzi wa wanajamii ambao watakuwa tayari kuhudhuria kikao cha majadiliano. Ikiwa wanachama wote wanataka kushiriki, mwezeshaji atamshauri kiongozi wa jamii kuja na vigezo vya uteuzi wa washiriki wa kikao cha majadiliano.

Mialiko inapaswa kuwa wazi na kutolewa kwa wakati (zaidi ya wiki moja kabla) ili kuepuka mkanganyiko. Mialiko inaweza kuwa kupitia barua

au ujumbe wa mdomo kutoka kwa mtaalam katika Mamlaka za Serikali za Mitaa au mashirika ambayo yanawezesha majadiliano ili kuthibitisha uhalali.

Mwaliko unapaswa kujumuisha tarehe kamili, mahali, muda pamoja na mada na kwa nini wamealikwa. Ikibidi kwa wanawake, wasichana na wavulana, unaweza kutaka kumhakikishia mkuu wa kaya kwamba hii ni shughuli halali ya elimu ambayo imeidhinishwa na Serikali.

#### 4.1.3. Utambulisho wa Mahali pa Kufanyia Majadiliano

Majadiliano ya ngazi jamii yanaweza kufanyika katika maeneo na miundo mbalimbali. Inaweza kuhusisha watu watano hadi watu mia moja au zaidi wanaohudhuria mkutano wa kijiji. Utambulisho wa mahali pa majadiliano ngazi ya jamii unapaswa kuhusisha jamii yenyewe. Wakati wa kuchagua mahali pa kufanyia majadiliano, ni muhimu kwa mratibu kuzingatia yafuatayo:

- Je, mahali pa kufanyia majadiliano ni salama - na panatoa nafasi kwa ajili ya usiri na faragha ya washiriki?;
- Je, nafasi hii inapatikana kwa washiriki? Kwa mfano, baadhi ya maeneo yanaweza kuwa na vizuizi vitakavyosababisha wazee/watu wenye ulemavu kushindwa kuhudhuria, ilhali kumbi zingine zinaweza kuwa za hadharani

zaidi kwa baadhi ya wanawake ambao wanataka kuweka hadhi ya chini;

- Je, viti vinastarehesha?;
- Je, viti vinaweza kupangwa kwenye duara? Kupanga viti katika duara ni muhimu kwani hutoa hali ya usawa miongoni mwa washiriki, inaruhusu washiriki kutazamana ana kwa ana na kuhimiza majadiliano ya wazi;
- Je, ni bajeti kiasi gani inapatikana kwa ajili ya majadiliano ngazi ya jamii?; na
- Je, ni muda kiasi gani umepangwa kwa ajili ya kuwezesha majadiliano ngazi ya jamii?

Baadhi ya mifano ya mahali ambapo majadiliano yanaweza kutokea:

- Kwenye chumba cha darasa la shule;
- Katika soko;
- Katika chumba cha mikutano;
- Ukumbi wa jumuiya/jamii au Kituo cha Maarifa;
- Katika sehemu za ibada; na
- Katika kumbi za mikutano za mashirika yaliyopo.

Maeneo ya kisiasa na makazi ya watu yanapaswa kuepukwa kwani hii inaweza kubadilisha maudhui ya vikao na uhusiano wa mamlaka ndani ya chumba. Katika baadhi ya jamii, kumbi na ratiba mbalimbali zitahitajika ili kuwashirikisha wadau

wenye ratiba au mitindo tofauti ya maisha.

### 4.1.4. Uteuzi wa Mbinu na Zana za Uwezeshaji

Uteuzi wa mbinu zinazofaa huwezesha majadiliano yenye mafanikio ambayo yanahimiza mbinu za uzoefu na shirikishi. Kulingana na mbinu iliyochaguliwa, ni muhimu kuhakikisha kuwa zana zitakazotumika katika mchakato wa majadiliano zinaendana na mbinu iliyochaguliwa na zinapatikana kwa urahisi katika jamii. Zana zinazohitajika zinapaswa kuandaliwa mapema.

### 4.1.5. Muda wa Majadiliano

Mazungumzo yanahitaji muda mzuri ambao unazingatia ratiba ya kila siku ya mshiriki. Wawezeshaji wanapopanga majadiliano wanapaswa kuzingatia masuala yote yanayozunguka kalenda ya msimu katika jamii inayolengwa. Kuamua muda wa kufanya majadiliano ngazi ya jamii inapaswa kuzingatia makubaliano kati ya jamii na mwezeshaji.

Muda unaotumika kwa ajili ya kikao cha majadiliano usiwe mrefu sana. Inashauriwa kutumia saa tatu (3) hadi nne (4) kwa siku kulingana na lengo la jumla na idadi ya vikao vilivyopangwa kufanywa katika kujadili mila na desturi fulani katika jamii.

### 4.1.6. Huduma Zinazopatikana

Utafiti mdogo kuhusu huduma zinazopatikana karibu na ukumbi (miundo ya usaidizi wa jamii, wasaidizi wa kisheria, afya, ulinzi wa mtoto/kinga ya jamii na polisi) lazima ufanywe mapema kabla ya majadiliano. Uelewa kuhusu huduma zinazopatikana karibu na eneo la ukumbi husaidia pale mshiriki yeyote anapohitaji kuunganishwa na huduma hizo. Katika baadhi ya matukio, wakati wa vikao vya majadiliano, mwezeshaji anaweza kukabiliwa na hali isiyo ya kawaida ambapo washiriki wanaweza kuonesha waziwazi kuathirika kihisia kutokana na madhila mbalimbali waliyokutana nayo katika maisha yao. Katika tukio la mwathirika au mwanafamilia wa karibu anayehitaji usaidizi, mwezeshaji anapaswa kuwa na kanzidata ya wanasihi, wataalam wa afya/matabibu au vituo au nyumba salama ambapo waathirika au washiriki wanaweza kupelekwa kwa ajili ya matibabu au uangalizi, ulinzi wa mtoto, ulinzi wa kijamii au usaidizi kutoka kwa polisi.

### 4.1.7. Kukamilisha Maandalizi ya Mada za Kikao

Kabla ya kuanza kwa kipindi, mwezeshaji atahitaji kufanya mapitio ya mpango wa kipindi kwa muhtasari wa kina kwa kuzingatia hatua zifuatazo:

- Maudhui ya mada kwa ajili ya majadiliano
- Malengo
- Muda wa kikao
- Rasilimali zinazohitajika

- Maandalizi ya mapema kuhusu eneo la kikao
- Muhtasari wa majadiliano hatua kwa hatua:-
  - ❖ Hatua ya 1: Utambulisho wa washiriki (wafahamiane kwa majina)
  - ❖ Hatua ya 2: Utangulizi wa kipindi
  - ❖ Hatua ya 3: Maelezo ya shughuli kuu zenye mbinu kulingana na mifano iliyoainishwa katika Sehemu ya 3 na Kiambatisho Na. 2)
  - ❖ Hatua ya 4: Kufunga kipindi

Kulingana na mahitaji ya hadhira, jinsi, umri, ulemavu na kiwango cha kujua kusoma na kuandika, baadhi ya shughuli zinaweza kubadilishwa ili ziwe rafiki zaidi.

## 4.2. Kuendesha Majadiliano Ngazi ya Jamii

### 4.2.1. Kuwasili, Kujiandikisha na Kuketi

Baada ya kuwasili kwenye ukumbi wa majadiliano, shughuli za awali zinazohusisha masuala ya usajili zitakamilika haraka iwezekanavyo. Ni muhimu kukusanya taarifa nyingi iwezekanavyo kuhusu historia ya mshiriki ili kuweza kufanya ufuatiliaji baada ya majadiliano kwa ajili ya kumbukumbu na mialiko ya vikao vitakavyofuata.

Kuwa na mwonekano chanya na tulivu kabla ya kuanza majadiliano ni ufunguo wa kufanikisha kipindi. Hili linaweza kufanyika kabla ya kufungua majadiliano kwa mwezeshaji kuwasalimu washiriki

kwa uchangamfu wanapowasili, kujifunza majina yao, kupanga alama zinazoeleweka na kuwapa viburudisho vyepesi. Kuhakikisha watu wanajisikia vizuri wanapowasili na kuwaeleza washiriki umuhimu wa uwepo wao. Hii inaunda hali ambayo itawahimiza washiriki kujenga uaminifu na kujitolea.

Hakikisha kwamba kila mtu ameketi kwenye ngazi sawa (iwe kwenye sakafu au ameketi kwenye viti) kwenye duara. Hii inahakikisha hali ya usawa katika chumba. Pia kuwa katika duara bila meza mbele ya washiriki kunahimiza mawasiliano ya ana kwa ana katika kikundi husika na kuwezesha ushiriki zaidi.

Mwezeshaji anapaswa kujiandaa kwa ajili ya kuhakikisha uwepo wa washiriki watu wenye ulemavu hata kama hawakualikwa na kuweza kukidhi hitaji lao la usaidizi ili kuhakikisha mchakato jumuishi.

**4.2.2. Kuanza Majadiliano**

Majadiliano yaanze kwa ufunguzi rasmi wa Kiongozi aliyepo ukumbini. Hii ni kwa sababu miundo ya uongozi wa jamii inaongoza juu ya kile ambacho ni cha manufaa, na kuzingatia mila na desturi nzuri za jamii. Uwepo wa viongozi wa jamii au maafisa wa utawala kufungua matukio ya majadiliano ngazi ya jamii huongeza imani ya jamii katika tukio husika.

Kiongozi afahamishwe mapema kuhusu madhumuni ya tukio na aina ya washiriki. Inafaa zaidi ikiwa inawezekana kupata muda wa mazungumzo ya ana kwa ana. Bila maelezo mafupi, kunaweza kusababisha kiongozi kupotosha madhumuni ya matukio na kusababisha mkanganyiko. Tukio hilo lisitumike kukuza ajenda ya kisiasa.

### 4.2.3. Kuanzisha Ajenda na Mbinu za Majadiliano

Wapitishe washiriki katika ajenda na utambulishe malengo, mbinu na ratiba ya vipindi. Mjadala unatakiwa kueleza kwa uwazi mwelekeo wa majadiliano na kuwafahamisha washiriki kuwa mada kuu ni mila na desturi katika jamii.

Fungua mkutano kwa kutoa maelezo ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Pia zungumzia na kutoa ufafanuzi kuhusu mila na desturi chanya na zile zenye madhara katika jamii na hali ilivyo hapa nchini Tanzania. Elezea athari za muda mrefu kwa mwathirika wa ukatili, athari katika ngazi ya familia na maendeleo ya mtoto. Aidha, zungumzia athari za mila na desturi zenye madhara katika maendeleo ya nchi kwa ujumla.

- Sisitiza kwamba hakuna anayestahili kuwa mwathirika wa ukatili wa kijinsia au ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

- Ni wajibu wa kila mtu kuzuia ukatili na/au kutoa huduma kwa waathirika wa vitendo vya ukatili.

### 4.2.4. Matarajio ya Washiriki na Kuunda Kanuni za Msingi

Tumia muda wa dakika chache kupata matarajio ya washiriki na yahusishe na majadiliano yanayotarajiwa. Kadhalika, tambua hofu za washiriki na uzishughulikie kwa undani. Kisha waongoze washiriki kuunda kanuni za msingi zitakazoongoza majadiliano yenye ufanisi. Kanuni za msingi zinalenga kuhakikisha uwepo wa mazingira salama, heshima, kujali, usiri pamoja na uhuru na uwazi katika majadiliano. Saidia kikundi kupata kanuni muhimu za msingi zinazoonekana kuwa muhimu kama vile usiri na kuheshimu maoni au mawazo ya watu wengine.

Tumia mbinu maalum zitakazoshawishi ushiriki mpana na wa wazi katika majadiliano. Hili linaweza kufanywa kupitia baadhi ya maswali rahisi ya utangulizi kama vile "Kwa nini mkutano huu ni muhimu kwako?" au “Ni nini kinachopaswa kufanyika hapa leo ili mkutano huu ufanikiwe?” Ruhusu kila mshiriki katika chumba kujitambulisha na baadaye unaweza kusisitiza jambo na kutoa maelezo mafupi itakapohitajika. Hii inajenga hisia kwamba mawazo na sauti za washiriki zinathaminiwa katika kikundi.

### 4.2.5. Kuanza kwa Majadiliano

Fuata na zingatia mpango wa shughuli za kipindi na hakikisha mada za majadiliano zinaendana na malengo ya kipindi.

Kumbuka kwamba kila mtu ana imani yake kuhusu majukumu ya wanaume na wanawake. Mara nyingi, mitazamo hiyo inaweza kukinzana. Ni muhimu kuheshimu imani ya mtu binafsi, lakini pia kukosoa zile ambazo zinaweza kuleta madhara kwa mtu huyo au kwa wengine. Hakikisha kuwa lengo la majadiliano sio kumfanya mtu yeyote ajisikie kuwa na hatia kutokana na kuathirika na vitendo vya ukatili, au kutotekeleza wajibu wake ipasavyo kuzuia ukatili katika siku za nyuma. Pia, lengo si kuwalaumu wanaume kwa ujumla au kujaribu kubaini watu walioendeleza ukatili. Badala yake, ni kutazama na kujipanga kwa siku zijazo na kuona ni nini zaidi tunaweza kufanya ili kubadilisha na kusaidia kuzuia vitendo vya ukatili katika jamii zetu.

Wakati wa majadiliano, mwezeshaji lazima azingatie na kuwa makini na majibu ya washiriki kwa sababu kuna uwezekano wa kuwakumbusha madhila ya vitendo vya ukatili ambavyo wamewahi kukumbana navyo hapo awali au walipokuwa watazamaji na hawakufanya jitihada za kutosha kuzuia ukatili. Endapo mshiriki atafichua madhila aliyokumbana nayo wakati wa kikao, mtambue mshiriki huyo, mhakikishie usalama wake na

wakumbushe kundi kubwa kuhusu umuhimu wa kuzingatia kanuni ya usiri. Pata muda wa kuzungumza na mshiriki aliyefichua na umuunganishe na watoa huduma husika mapema na haraka iwezekanavyo.

### 4.2.6. Mpango Kazi wa Utekelezaji baada ya Majadiliano

Mwishoni mwa kila majadiliano, mwezeshaji anapaswa kuwawezesha washiriki kutoka na maazimio ya utekelezaji, ambayo yatajikita katika kushughulikia mila na desturi zenye madhara na kukuza mila na desturi chanya. Kwa hiyo, washiriki watapaswa kuandaa mpango kazi wa utekelezaji kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Na. 4.

### 4.2.7. Itifaki ya Kuhitimisha Majadiliano

Ili kuhakikisha uendelevu wa dhamira ya jamii kuchukua hatua, ni vyema mwezeshaji na/au waandaaji wa majadiliano ngazi ya jamii wakahitimisha majadiliano kwa namna bora na kufuata utaratibu unaofaa. Kuna mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa kuhitimisha majadiliano ili kuondoka kwenye jamii husika. Mambo hayo ni pamoja na:

- Kujadili mpango kazi ulioandaliwa na washiriki na kuuweka katika mtazamo unaoweza kutekelezeka;
- Kuendesha kikao rasmi cha kuagana ambacho kinaweza kujumuisha kuwaalika viongozi;

- Kuendesha kikao cha majumuisho na viongozi ili kuwasilisha;
    1. Yaliyojiri wakati wa majadiliano,
    2. Maazimio na mipango kazi ya washiriki na msaada wanaoweza kuhitaji ili kufanikisha utekelezaji wake,
    3. Mpango wa baadaye katika usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya mada za majadiliano.

Kikao cha mrejesho kwa mamlaka husika kuhusu majumuisho ya mada zilizotolewa wakati wa majadiliano, kitasaidia kuandaa mpango wa utoaji taarifa za utekelezaji wa mipango kazi ya washiriki.

**4.2.8. Ufuatiliaji na Kuendeleza Majadiliano**

Mchakato wa kubadilisha mila na desturi katika jamii zinazohusu usawa wa kijinsia, ukatili dhidi ya wanawake na watoto huchukua muda na huhitaji uwekezaji na majadiliano endelevu. Kadiri inavyowezekana na rasilimali fedha na muda zitakavyoruhusu, majadiliano yaendelezwe kwa kuwezesha majadiliano ngazi ya jamii kufanyika zaidi ya mara moja. Awamu ya majadiliano itakayofuata inaweza kujumuisha utambulisho wa mada mpya, mazoezi, au vikundi vya wadau ngazi ya jamii, muhtasari/marejeo ya vipindi vya majadiliano vilivyopita au kufuatilia utekelezaji wa

mipango kazi iliyoandaliwa wakati wa majadiliano yaliyopita (Angalia Sura ya 5).

# SURA YA TANO

## UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Utunzaji wa kumbukumbu, ufuatiliaji na tathmini ni muhimu ili kuboresha ufanisi wa majadiliano ngazi ya jamii. Ufuatiliaji makini huruhusu watekelezaji au waandaaji kufanya maamuzi yanayofaa siku hadi siku na kuhakikisha kwamba afua zinatekelezwa kama zilivyopangwa na kurekebishwa inapobidi.

Tathmini huwawezesha watekelezaji au waandaaji wa majadiliano kuelewa na kuonesha matokeo ya kazi zao, kuamua mikakati bora ya kufikia malengo yao na kuweka kumbukumbu ya mambo muhimu waliyojifunza ili kuboresha majadiliano kwa siku zijazo.

### 5.1. Utunzaji wa Kumbukumbu za Majadiliano

Kimsingi, mtu binafsi au mwezeshaji mwenza ni lazima atambuliwe kutoka katika kikundi ambaye atakuwa na jukumu la kuchukua muhtasari na kutunza kumbukumbu za masuala yote muhimu yanayohusu vipindi vya majadiliano. Itakuwa ni jambo jema na la kuvutia kuhusisha vyombo vya habari ambavyo vitaandika mchakato na vitaweza kuchukua picha mnato na picha mjongeo kwa ajili ya kumbukumbu. Hii inaweza kutumika kama

nyenzo ya marejeleo kwa vipindi vyovyote vya baadaye au marudio ya vipindi vya majadiliano.

### 5.2. Kutathmini Matokeo

Inapendekezwa kufanyika kwa tathmini ya kupima uelewa wa washiriki kabla na baada ya vipindi vya majadiliano ngazi ya jamii vinavyochunguza mila na desturi kuhusiana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto na ukatili wa kijinsia. Tathmini zitakuwa za aina mbili, moja itawalenga washiriki wanaojua kusoma na kuandika na nyingine kwa washiriki wasiojua kusoma na kuandika. Majaribio haya ya kabla na baada (pamoja na karatasi za majibu) yanapatikana katika Kiambatisho Na. 5.

Tathmini shirikishi mwishoni mwa kipindi cha majadiliano itawezesha yafuatayo:

- Itawapa washiriki fursa ya kutoa maoni au mawazo yao kuhusu mchakato na mwenendo wa majadiliano;
- Itawapa washiriki nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu jinsi kipindi cha majadiliano kilivyowezeshwa; na
- Itatoa fursa kwa mwezeshaji kufahamu kama washiriki walielewa vyema mada zilizowasilishwa na endapo ujumbe umewafikia walengwa.

Katika muda wa kati hadi mrefu, tathmini zinaweza kuwa muhimu katika kupima:

- Hali ya utekelezaji wa mpango kazi;
- Ufanisi wa majadiliano ngazi ya jamii kwa kuzingatia matarajio ya jamii na matokeo ya muda mrefu;
- Iwapo kuna mabadiliko katika maarifa, mtazamo, imani na desturi, kwa mfano, mabadiliko ya mila na desturi katika jamii zinazotoa fursa sawa kwa wanawake na wasichana kushiriki katika kufanya maamuzi ndani ya kaya na jamii; na
- Kama afua ni endelevu.

Tathmini zinaweza kuandikwa na/au kuelezwa kwa maneno. Chagua zana zinazofaa za kukusanya taarifa, kama vile, madodoso, mahojiano, mijadala ya vikundi lengwa na rejista ya washiriki.

Baada ya kukamilika kwa zoezi la tathmini ya majadiliano ngazi ya jamii, wakala wa utekelezaji/mratibu wa majadiliano lazima awasilishe taarifa kwa mamlaka husika ya Serikali katika eneo lao kwa kutumia Fomu zinazopatikana katika Kiambatisho Na. 3.

## HITIMISHO

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WMJJWM) na Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid) Tanzania, walifanya utafiti kwa lengo la kujua mila na desturi ambazo zina mtizamo chanya kwa jamii na zitakazoweza kubadilisha tabia na mtizamo hasi kwa lengo la kuondoa mila zenye kuleta madhara kwa jamii. Aidha, hii inaendana na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18 – 2021/22. Pia, utafiti huo ulionesha masuala ya kijinsia yanayohusiana na tamaduni, mila na desturi ambazo zinawakandamiza wanawake na watoto. Ni kwa sababu hiyo kuna haja ya kufanya majadiliano juu ya tamaduni, mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii ili kufikia lengo lililokusudiwa.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATISHO NA. 1: MILA NA DESTURI ZITAKAZOHUSISHWA WAKATI WA MAJADILIANO YA JAMII ZINAZOSABABISHA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO

1. Kuanzisha vikundi vya wanawake na wanaume katika jamii ambavyo vitajihusisha na majadiliano juu ya usawa wa kijinsia katika jamii.
2. Kujenga uelewa wa pamoja kuhusu madaraka na mahusiano katika familia na jamii.
3. Kutokomeza ndoa za utotoni katika jamii.
4. Kutokomeza ukeketaji kwa wanawake na watoto wa kike katika jamii.
5. Kutokomeza mimba za utotoni katika jamii
6. Kuchukua hatua dhidi ya aina zote za ukatili wa kijinsia ikiwa ni pamoja na ukatili wa vipigo, ngono, kisaikolojia na kiuchumi katika jamii.
7. Kuchukua hatua dhidi ya ukatili kati ya wandoa.
8. Kuchukua hatua dhidi ya ukatili kwa watoto.
9. Kushirikisha jamii katika kutambua mila na desturi zinazochangia ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto.

## KIAMBATISHO NA. 2: MFANO WA UTARATIBU WA MAJADILIANO

Zipo shughuli mbalimbali ambazo zitawezesha majadiliano katika jamii. Shughuli hizo zitawezesha jamii kuwa na jukwaa la kutoa maoni yao, kuchambua na kuwa na mpango wa kuleta mabadiliko chanya ya tabia katika jamii.

Mifano inayoweza kutumiwa na mwezeshaji kama kichocheo cha kutengeneza mpango wa mikutano/majukwaa ya majadiliano kama ilivyotajwa katika sura ya tatu na ya nne ya Mwongozo huu ni kama ifuatavyo:

### MADA1: Mila Zinazosababisha Ubaguzi na Ukatili wa Kijinsia

**Lengo**

Baada ya majadiliano, washiriki wataweza kuwa na uwezo wa:

1. Kuelezea tofauti ya “jinsi” na “jinsia”, ‘usawa wa kijinsia na haki sawa za kijinsia”.
2. Kuelezea mila zisizokuwa na usawa wa kijinsia na matokeo yake kwa wanaume, wenzi wao na familia zinazohusu ukatili wa kijinsia, ndoa za utotoni, ukeketaji, hali hatarishi ya kupata maambukizi ya VVU, mimba za utotoni na matokeo hasi ya afya ya uzazi.

3. Elezea jinsi ambavyo wanaume na wanawake wanaweza kushirikiana ili kuleta usawa wa kijinsia na hivyo kutokomeza ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya wanawake na watoto na hali hatarishi ya maambukizi ya VVU.

**TANBIHI:**
Ili makundi mbalimbali ya kijamii yaweze kupata maarifa kuhusu jinsia, itagemeana na muda utakaotolewa kwa ajili ya wao kujifunza, hasa ikizingatiwa kuwa sio wanajamii wote wana uelewa kuhusu dhana za jinsia. Kwa hiyo muda wote uliopangwa kwa ajili ya majadiliano ni lazima utumike ipasavyo. Ni lazima muwezeshaji adodose ili kuhakikisha kuwa wanajamii wote wanakubaliana na maana ya maneno “jinsi” na “jinsia”.

**Maswali ya Majadiliano**

Maswali yafuatayo yanaweza kuulizwa ili kuwezesha majadiliano:

- Ni kitu gani ambacho kinachotofautisha mwanawake na mwanaume?
- Uliza washiriki iwapo wamewahi kuambiwa kuwa wafanye vitu kama “mwanaume/mwanamke”. Waulize iwapo wana uzoefu wa mtu ambaye amewahi kusema maneno kama hayo, na wanafikiri ni “kwa nini alisema hivyo?” “Ulijisikiaje?” “Je,

kuna mabadiliko kwa kadiri muda unavyopita?" *(Wasisitize washiriki kutoa mifano mingi iwezekanavyo inayoeleza vitu ambavyo mwanaume/mwanamke anaambiwa katika jamii kuhusu namna anavyotakiwa kuwa/kuishi).*

- Unaweza kufikiri namna ambavyo umekuwa ukichukuliwa/kuthaminiwa kwa namna tofauti kwa sababu wewe ni mwanamke/mwanaume?
- Ni mambo gani yanayojitokeza ambayo ni matokeo ya tofauti kati ya mwanaume na mwanamke kulingana na jinsi ambavyo wamelelewa au kufundishwa na familia/jamii?
- Ni nini tofauti kati ya "jinsia" na "jinsi"? Je, unaelewa maana ya dhana hizi mbili? *(Dodosa ili uone iwapo kikundi/ washiriki wanafikiri kuwa tofauti hizi mbili ni za kibaolojia au zimetengenezwa na jamii).*

Baada ya kupata mrejesho kutoka kwa washiriki, elezea tofauti kati ya jinsia na jinsi. Tumia mifano iliyotolewa na washiriki wakati wa kipindi cha majadiliano.

- Uliza iwapo matarajio ya matokeo ya muda mfupi kwa jamii kwa wanaume na wanawake yatakuwa ya usawa? Je, kuna kundi ambalo halitatendewa haki? Ni nini matarajio (katika

imani, tamaduni, na utekelezaji wake) katika jamii zetu zinazowafanya wanaume na wanawake kutokuwa na usawa wa madaraka?

- Elezea usawa wa kijinsia na haki sawa za kijinsia na toa mifano inayoonesha namna ambavyo kutokuwa na usawa wa kijinsia kunachangia kutokuwa na usawa wa madaraka na hivyo kusababisha ukatili.
- Waambie washiriki wafikiri yale waliyoyajadili. Je, wanafikiri hali hiyo itabadilika? Kama haitabadilika, kwa nini, kama itabadilika je, kuna uwezekano wa hali hiyo kubadilika? Kwa namna gani/kwa vipi?
- Ni jinsi gani mtu binafsi, viongozi mashuhuri, wazazi, mashirika, wafanyibiashara, shule, vyombo vya habari n.k, wanaweza kushirikishwa katika kuwezesha uwepo wa mila zinazoleta usawa kwenye jamii?
- Je, washiriki wanaweza kuwa sehemu ya kuleta mabadiliko hayo? Ni kitu gani ambacho sisi binafsi tunaweza kufanya leo ili kubadilisha mila kandamizi katika mahusiano yetu na ya jamii?
- Sikiliza majibu ya washiriki na wahimize kutaja mabadiliko madogo katika maisha yao ya kila siku.
- Washukuru washiriki kwa muda wao walioutoa na ufunge kipindi.

**Neno la Kufunga Mjadala/Kipindi**

Siku zote katika maisha yetu, wanaume na wanawake wanapokea taarifa tofauti kutoka katika familia, vyombo vya habari na jamii kuhusu jinsi ambavyo wanatakiwa waishi na namna ya kushirikiana na wengine (mfano: “wavulana kupigana, wasichana kupika”). Tofauti hizi nyingi hutengenezwa na jamii na sio sehemu ya maumbile ya kibaologia. Mtazamo wa jamii kuhusu mtu kuwa mwanamme au mwanamke wakati mwingine imekuwa ni silaha ya kuchochea na kuendeleza ukatili katika jamii na kuwaweka wanaume na wanawake katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU.

Mara nyingi watu hususan wanaume wanaweza kuchagua kuishi maisha wanayotaka kwa kujiamini na kuwa huru katika hizi sheria/tabia kwa kuanza kuelewa mateso ambayo yanasababishwa na kutokuwa na usawa katika jamii kunakosabibishwa na mila na desturi ambazo hazitoi haki sawa kwa wote; na ambazo zinawaweka wanaume wenyewe, wenzi wao na familia zao katika hatari ya ukatili wa kijinsia na maambukizi ya VVU. Familia ambazo hazina ukatili wa kijinsia wanaishi maisha ya furaha na kuwa na afya nzuri. Ni jukumu la kila mtu kuchukua hatua kuzuia mila na desturi zenye kuleta madhara. Ni lazima kila mtu ajue jukumu lake na kuchukua hatua.

## MADA YA 2: Kuelezea Uhusiano wa Mabadiliko ya Madaraka ya Kijinsia kati ya Watu na Vitu

### Lengo

Mwisho wa majadiliano washiriki waweze kuwa na uelewa kuhusu uwepo wa madaraka katika mahusiano na matokeo yake kwa mtu binafsi.

### Muhtasari wa Mwezeshaji

Baadhi ya washiriki wanaweza wasijisikie vizuri kushiriki katika igizo la shughuli hii. Ni muhimu kuwa mwangalifu na kujua jinsi ambavyo washiriki wanajisikia (hisia) wanapopewa jukumu la kuwa "mtu" au "kitu" na mwezeshaji awe tayari kuchukua hatua na kufanya mabadiliko muhimu. Kwa mfano, badala ya washiriki kufanya lile igizo, mwezeshaji anaweza kuwaambia washiriki wajadili wawili wawili jinsi ambavyo "watu" wanaweza kuchukulia "vitu" na hisia zinazoweza kujitokeza kwa "watu" na "vitu". Pia ni lazima mwezeshaji ajiandae kwa ajili ya kuwa na eneo la rufaa kwa ajili ya ushauri nasaha au huduma zingine kwa ajili ya washiriki ambao wanaweza kuathiriwa na shughuli hii.

### Mchakato

- Gawanya washiriki katika makundi ya watu watatu.
- Wajulishe washiriki kuwa jina la shughuli hiyo ni: Watu na Vitu. Katika kila kundi,

mshiriki mmoja anakuwa “kitu” mwingine “mtu” na wa tatu awe “mtazamaji”.

- Soma maelekezo yafuatayo kwa ajili ya kundi:

**VITU**: Huwezi kufikiri, kuhisi, au kufanya maamuzi. Unatekeleza yale ambayo umeambiwa na “mtu”. Kama unataka kwenda mahali au kufanya kitu fulani, ni lazima uombe ruhusa kwa yule “mtu” ufanye.

**WATU**: Una uwezo wa kufikiri, kuhisi, na unaweza kufanya maamuzi. Zaidi ya hapo, unaweza kumwambia “kitu” afanye nini.

**MTAZAMAJI**: Unatazama kila kitu kinachotokea na unabaki kimya.

1. Mwambie kila “mtu” kulazimisha “kitu” na kuwaambia wawaambie “kitu” kitu cha kufanya (wakiwa ndani ya chumba).
2. Wape vikundi dakika tano kwa ajili ya “mtu” na “kitu” kufanya majukumu yao.
3. Baada ya dakika tano, waambie watu na vitu kwamba wabadilishane majukumu na kwamba sasa “watu” watakuwa “vitu” na “vitu” vitakuwa “watu”. Wape dakika tano zingine za kutekeleza majukumu yao.
4. Mwisho, waambie washiriki kurudi katika sehemu zao hapo katika chumba cha semina

na watumie yale maswali ya mfano yafuatayo katika kuendeleza majadiliano:

- Je, “mtu” wako anakuchukuliaje (treat)? Unajisikiaje? Unahisi kama huna mamlaka? Kwa nini ndio au hapana?
- Unachukuliaje “vitu”? Unasikia hisia gani kumfanyia mtu mwingine hivyo? Unawachukuliaje, Unajisikiaje kumchukulia mwingine hivyo? Ili kufanya uwe na madaraka? Kwanini ndiyo au hapana?
- Kwa nini “vitu” vinatii na kufuata maelekezo yanayotolewa na “watu”?
- Je, kuna “vitu” au “watu” ambao walikataa kufanya hili zoezi?
- Je, katika maisha yako, kuna watu wengine ambao wanakuchukulia wewe kama “vitu”? Ni nani? Kwa nini? Katika maisha yako ya kila siku unawachukulia watu wengine kama “vitu”? Nani? Kwa nini?

**“Kwa Mtazamaji”:**

- Unajisikiaje kwa kutokufanya kitu chochote? Je, unajisikia kama unaingilia kile kilichotokea? Kama ndio, unafikiri ungefanya nini?
- Katika maisha yetu ya kila siku, sisi ni “watazamaji” wa hali ambayo baadhi ya watu ambao wanawachukulia wengine kama vitu?

Je, tunaingilia kati/tunachukua hatua? Kwa nini au kwa nini hatuchukui hatua?

- Kama ungepewa nafasi ya kuchagua kati ya majukumu matatu ni jukumu lipi ambalo ungelichagua na kwa nini?
- Kwa nini watu wanafanyiana hivyo?
- Ni nini matokeo ya mahusiano pale ambapo mtu mmoja anaweza kuwafanya wengine kama "kitu"?
- Ni kwa vipi mtu anapolinganishwa na "kitu" inamuweka katika hali hatarishi ya kupata VVU na mambo mengine yanayohusiana na afya?
- Katika jamii yako:
  - ❖ Je, mara nyingi wanaume wanaangukia katika makundi haya matatu? Kundi lipi?
  - ❖ Je, mara nyingi wanawake wanaangukia katika makundi haya matatu? Kundi lipi? Kwa nini unafikiri hivyo?
- Ni kwa namna gani jamii au tamaduni zinaendeleza au kusaidia kuendeleza aina hizi za mahusiano?
- Nini kifanyike ili kuhakikisha kuwa makundi tofauti kama ya wanaume na wanawake wanaishi katika dunia ya usawa ambayo wanaweza kufurahia fursa sawa, usawa wa huduma/kuhudumiwa na haki sawa?

**Muhtasari wa Kufunga**

Kuna aina nyingi za mahusianao ambayo mtu mmoja anaweza akawa na madaraka/mamlaka juu ya mwingine. Kutokuwa na uwiano wa madaraka kati ya wanaume na wanawake katika uhusiano wa wanandoa inaweza kusababisha matokeo hasi ambayo yanaweza kuchangia katika maambukizi ya magojnwa ya zinaa, VVU na UKIMWI na mimba ambazo hazijapangwa. Kwa mfano, mara nyingi mwanamke hana mamlaka ya kuamua ni lini, wapi na kwa vipi tendo la ndoa lifanyike, ikiwa ni pamoja na kutumia kondomu kwa sababu ya imani ya muda mrefu kuwa mwanaume anatakiwa awe na nguvu za kutosha linapokuja suala la tendo la ndoa na mwanamke anatakiwa awe anakubaliana na matakwa ya mwanaume.

Kwa maneno mengine, mwanamke ambaye anamtegemea mume wake kwa ajili ya fedha/kipato anaweza kujisikia kuwa hana mamlaka/uwezo wa kusema hapana kuhusu tendo la ndoa. Pale ambapo wanandoa wanatofautiana sana kwa umri, au viwango vya maisha kati ya wanaume na wanawake inaweza kusababisha tofauti kubwa ya madaraka katika uhusiano ambayo inasababisha hali hatarishi kati yao. Ipo mifano mingine ya mahusiano katika maisha yetu na katika jamii. Fikiria uhusiano kati ya vijana na watu wazima, wanafunzi na waalimu, waajiri na waajiriwa. Wakati mwingine kutokuwa na usawa katika mahusianao

yanaweza kusababisha mtu mmoja kumfanyia/kumfanya mwingine kama kitu. Kama mlivyojadili jinsia na mahusianao kati ya mwanaume na mwanamke, ni muhimu kukumbuka uhusiano kati ya namna mtu anavyojisikia anakandamizwa au anapofanyiwa kama "kitu" katika mahusianao mengine lazima kuangalia namana unavyowafanyia wengine wakiwemo wanawake kufanywa kama "kitu". Fikiri kuhusu kuwasiliana kunavyoweza kusaidia kujenga mahusiano yenye usawa kwa mwanamke nyumbani na katika jamii.

## MADA 3: Bakuli la Ukatili wa Kijinsia (GBV *Fishbowl*)

### Malengo

Kufikia mwisho wa majadiliano, washiriki waweze kufanya yafuatayo;

1. Kuelezea aina tofauti za maisha na uzoefu kati ya wanaume na wanawake.
2. Kuelezea namna ambavyo kutokukubaliana na mawazo ya jamii kwa mwanaume au mwanamke anavyotakiwa kuishi kunaweza kusababisha hali hatarishi katika ukatili wa kijinsia.
3. Jadili namna ambavyo wanaume na wanawake katika jamii wanaweza kuwa washirika wa kuendeleza usawa wa kijinsia kupitia mila nzuri

na kuondoa mila na desturi ambazo ni za ukatili na zinaleta madhara kwa jamii.

**Utangulizi**

- Wajulishe washiriki kuwa utaendesha kikao cha muda wa saa moja ambacho kinahusiana na mambo ya ukatili wa kijinsia, jambo ambalo lina madhara kiafya na utu wa wanajamii.
- Waeleze washiriki: "Tutafanya shughuli ambayo itaonesha maisha tofauti kati ya wanaume na wanawake".
- Wanawake wakae ndani ya duara wakati wanaume watakaa nje ya duara, Ongoza wanawake kujadili mambo ambayo yanawaathiri kwa kutumia maswali yafuatayo kwa wanawake.
- Wakati huu, wanaume hawaruhusiwi kusema chochote. Baada ya majadiliano ya kina ya wanawake, waambie wanaume wakae ndani ya duara na wanawake wakae nje ya duara.
- Rudia mchakato uliotumika hapo juu katika wanawake na uliza maswali kwa wanaume kama ifuatavyo hapo chini.
- Wakati huu wanawake hawaruhusiwi kusema chochote. Katika jamii zingine hasa wakati wanandoa wanashiriki katika kikao inaweza kuwa vigumu kwa wanawake kueleza ukweli wa hali halisi ya maisha wanayopitia mbele ya waume zao. Kwa hiyo itakuwa vizuri kuwatia

moyo kuongea mbele ya waume, na waongee kwa ujumla wakati wa somo/kipindi.

**Maswali ya Majadiliano**

**Maswali kwa Wanawake:**

1. Ni jambo gani gumu sana unalopitia katika jamii kwa sababu tu wewe ni mwanamke?
2. Ni jambo gani gumu unaloliona katika kuwaelewa wanaume katika jamii yako?
3. Ni kwa namna gani maneno ambayo wanaume wanasema au jamii inayaamini kuhusu wanawake na ambayo yanaathiri maisha ya wanawake?
4. Ni kitu gani kinatokea pale ambapo mwanamke haishi maisha ya kukubaliana kuwa ni mwanamke? (Majibu yanaweza kuwa: kipigo au kuumizwa mwili kwa namna nyingine, kutukanwa au kunenewa kauli mbaya za ukali, kudhalilishwa/kuaibishwa, kufukuzwa, 'adhabu zingine').
5. Ni usemi upi mmojawapo ambao hupendi kuusikia wanaume au jamii ikiusema kuhusu wanawake?

Baada ya duara la ndani (wanawake) watakapomaliza kushirikishana mawazo yao, washukuru.

Wakumbushe duara la nje (sasa ni wanawake) kwamba sheria ya *gender fishbowl* ni kwa ajili ya wale ambao wamekaa nje ya mduara kwamba wao wanatakiwa kusikiliza tu.

**Maswali kwa Wanaume:**

1. Ni jambo gani gumu sana unalopitia katika jamii kwa sababu tu wewe ni mwanaume?
2. Ni jambo gani gumu unaloliona katika kuwaelewa wanawake katika jamii yako?
3. Ni kwa namna gani maneno ambayo wanawake wanasema au jamii inayaamini kuhusu wanaume na ambayo yanaathiri maisha ya wanaume? (Majibu yanaweza kuwa: muendelezo wa tabia za kimamlaka, kuwa na wapenzi wengi, walevi, n.k.)
4. Ni kitu gani kinatokea pale ambapo mwanamme haishi maisha ya kukubaliana kuwa ni mwanaume? (Majibu yanaweza kuwa matusi/kutukanwa, kudhalilishwa, au kuitwa bwege)
5. Ni usemi upi mmojawapo ambao hupendi kuusikia wanawake au jamii ikiusema kuhusu wanaume?

Waambie washiriki, wakiwemo watazamaji waangalie kila mtu katika nafsi yake aone kama kuna majibu ambayo hakuyatarajia kuyasikia kutoka pande zote.

1. Umejifunza nini kama matokeo ya majadiliano haya? Chunguza ni kwa namna gani haiendani na mawazo ya jamii kwamba ni kwa namna gani mwanaume au mwanamke anaweza kusababisha ukatili.
2. Je, inawezekana hali hii kubadilika? Kwa namna gani?
3. Utafanya nini tofauti kama matokeo ya zoezi hili?

Sikiliza majibu ya washiriki na kuwatia moyo kuonesha/kutaja mabadiliko madogo na makubwa katika maisha yao.

Washukuru washiriki kwa muda wao na kufunga kikao.

**Muhtasari wa Kufunga Kikao**

Kutoka utoto, familia, vyombo vya habari, na jamii huwasiliana na wanaume na wanawake kuhusu namna gani watafanya nini ili waweze kushirikiana na wengine. Tofauti nyingi zimejengwa na jamii na siyo sehemu ya asili. Maelezo ya jamii kuhusu uwanaume na uwanawake wakati mwingine ni dhana inayoendeleza ukatili kwa jamii na kuweka wanaume na wanawake katika hali hatarishi ya kupata maambukizi ya VVU.

Kama tulivyoona, hakuna mtu anayejishughulisha pale inapotokea ukatili wa kijinsia [mfano; mwanamke anapopigwa na mume wake kwa

sababu ya kuunguza chakula au mwanaume anapokuwa na wapenzi wengi]. Mada hii ya ukatili wa kijinsia kwa kutumia *fishbowl* imetupa nafasi ya kutoa mawazo na kusikia kutoka kwa wengine. Sasa tunajua baadhi ya vitu ambavyo ni vyanzo vya maumivu na kuteseka kwa wengine.

## MADA 4: Ndoa za utotoni

### Malengo

Kufikia mwisho wa kikao washiriki waweze kuelewa na kufanya yafuatayo;

1. Eleza maana ya ndoa za utotoni
2. Kueleza/kuonesha visababishi vya ndoa za utotoni
3. Eleza vihatarishi vinavyohusiana na matokeo ya ndoa za utotoni katika jamii
4. Onesha/eleza mikakati ambayo inaweza kutumiwa na jamii kuzuia ndoa za utotoni.

### Muhtasari wa Mwezeshaji

Unapoendelea kuwezesha kikao washiriki wakumbushwe kuwa kulingana na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa urekebu mwaka 2019, mtoto ni mtu yeyote mwanaume au mwanamke aliye na umri chini ya miaka18.

**Shughuli ya Kuibua Ndoa za Utotoni (*Child Marriage Visualization Activity*)**

Tambulisha shughuli hii kwa kuelezea kuwa kutokuwa na usawa wa madaraka kati ya wanaume na wanawake inawaweka wasichana katika hali hatarishi ya kuingia kwenye ndoa za utotoni. Hii ni kwa sababu ukilinganisha na wengine katika familia (hasa wavulana) wasichana wanaangaliwa kama wenye malengo madogo ya kulea watoto kwenye familia, kushughulika na maisha yao ya sasa na kutunza familia zao kwa kupika, usafi na kutunza waume na watoto wao. Wasichana wana nafasi/madaraka madogo katika kuchagua/kuamua lini na wapi aolewe.

Karibisha washiriki kukaa katika duara ambapo wataweza kusikiliza hadithi ya Lenganji. Mshiriki mmoja asome hadithi hiyo kwa sauti.

"*Habari, jina langu ni Lenganji, nina umri wa miaka 16. Ninaishi Nyangao. Niliolewa miezi sita iliyopita na mvulana mwenye umri wa miaka 17 kutoka kijiji kingine. Sijui kwanini niliolewa na kijana huyu mdogo kwa umri. Ninaishi na wazazi wangu hadi wakati wa sherehe za harusi hivyo sijui ni lini nitaenda kuishi nyumbani kwa mume wangu. Wakati ninapoulizwa kuhusu kuolewa na mume wangu natabasamu na sisemi chochote pamoja na kwamba nakasirika na kuogopa. Nafurahia shule na natamani kuwa mwalimu siku zijazo. Kama*

*nikiolewa sasa, nitatakiwa kuacha shule na kuanza kumtunza mume na kuzaa watoto. Wakati ninapowauliza baba na mama kuhusu kuchelewesha kuolewa kwangu wanasema, "Hivi ndivyo mambo yalivyo". Hatuwezi kukusaidia. Kama hutaolewa katika kipindi hiki watu watafikiri kuna kitu kibaya ndani yako na familia yako. Pia hatuna fedha za kuendelea kukusomesha, kwa hiyo unatakiwa uwe binti mzuri/mwema na usikilize wazazi wako."*

**Waulize Washiriki Maswali Yafuatayo:**

1. Ni nini ilikuwa sababu ya Lenganji kuolewa? Dadisi: Umaskini, mila na Imani za jamii, au kutokuwa na usawa wa madaraka/maamuzi.
2. Ni madhara gani ambayo yatatokea kwa Lenganji hasa katika elimu yake na katika malengo yake ya baadaye ya kuwa mwalimu iwapo ataolewa katika umri mdogo?
3. Wazazi wa Lenganji walikuwa wanamaanisha nini wakati waliposema "Hivi ndivyo mambo yalivyo"? *Dadisi*:
4. Je, unafikiri wazazi wa Lenganji walihisi pia kuwa hawana madaraka ya kufanya maamuzi? Kwa nini?
5. Je, hii hadithi ya Lenganji inafanana kwa kiasi gani na mambo ambayo umewahi kuona au kuyasikia/kuyapitia?
6. Kwa nini ndoa za utotoni ni hatari kwa wasichana wadogo? Kwa familia? Kwa jamii?

7. Ni kitu gani unaweza kufanya ili kuwajengea uwezo nyumbani? (Andika majibu kwenye *flipchart*)
8. Ni kitu gani unaweza kufanya kwa wanaume katika familia yako au jamii yako ili kuwajengea uwezo wasichana? (Andika majibu kwenye *flipchart*)
9. Ni njia zipi ambazo zinaweza kutumika ili kuzuia ndoa za utotoni kwenye jamii zao?

Baada ya majibu ya washiriki, elezea mikakati zaidi ambayo itaweza kutumika katika kuzuia ndoa za utotoni katika jamii:

- Kujengea uwezo wasichana kwa kuwapa taarifa, maarifa na kusaidia upatikanaji wa mitandao na elimu yenye ubora kwa wasichana.
- Kuhimiza maamuzi shirikishi kwa wanandoa, kubadilisha mila na desturi zenye kuleta madhara na kusaidia programu za jamii.
- Kuongeza vyanzo vya uchumi wa familia ili kupunguza shinikizo la ukosefu wa vyanzo vya mapato na hivyo kusababisha msukumo wa ndoa za utotoni.
- Kujenga uelewa na kuwafundisha watu kusimamia na kuendeleza mila ambazo hazina madhara kwa jamii.
- Kuelimisha wanafamilia wote (awareness raising) ikiwa ni pamoja na wanaume,

wanawake, wasichana, wavulana, wazee wa kiume na wa kike.

- Kutoa msaada wa kiuchumi na motisha kwa wasichana na familia zao.
- Kushirikisha wanaume katika jamii kwa kuwafikia katika maeneo maalum na ambayo mara nyingi wanakuwepo kama kwenye viwanja vya michezo, vituo vya huduma za afya, shule, maeneo ya ibada, maeneo ya huduma za umma na maeneo ya biashara ambazo zinatoa huduma za sherehe za harusi. Njia nyingine ni kuandaa mazungumzo katika jamii yanayohusisha upinzani chanya katika dini au taasisi za asili, watoa huduma za afya, mpangilio wa elimu na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kuboresha mazingira ambayo yanawezesha sheria na sera kutekelezwa: Kuhusishwa na kushirikishwa katika kusimamia na kutekeleza sheria. Polisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kupendekeza namna ya kutekeleza mawazo yaliyojadiliwa na jamii iwe na uwezo wa kuhoji utekelezaji wake.

**Muhtasari wa Kufunga**

Kutokuwa na usawa katika madaraka na maamuzi kati ya wanaume na wanawake inasababisha wasichana kuwa katika hatari ya kuolewa katika umri mdogo. Hii ni kwasababu wasichana wanatazamwa kuwa hawana jambo/lengo lingine

katika maisha yao bali wapo kwa ajili ya kuzaa watoto na kutunza nyumba zao za sasa na za baadae kwa kupika, kufanya usafi, kuwatunza waume na familia zao, matokeo yake wanakuwa na uwezo mdogo wa kiutawala na katika kufanya maamuzi kwamba ni lini na kwa makubaliano gani wataolewa. Kwa sababu hiyo kuna haja ya kuhakikisha kuwa jamii inawajengea uwezo wasichana katika kupata habari, maarifa, na kuwasaidia kupata mawasiliano na kuboresha mfumo wa elimu kwa wasichana; kwa hiyo ipo haja ya kuhimiza maamuzi shirikishi kwa wanandoa; kubadilisha mila na desturi zenye kuleta madhara na kusaidia programu za jamii ambazo zitaongeza vyanzo vya uchumi kwa familia ili kupunguza shinikizo linalosababisha ndoa za utotoni kwa wasichana.

## MADA YA 5: Ukeketaji

### Malengo.

Mwisho wa mjadala, washiriki wataweza kufanya yafuatayo:

1. Kuainisha sababu za kina na madhara ya ukeketaji kwa jamii zinazohusiana kutokuwepo usawa wa kijinsia; na
2. Kufikiria hatua sahihi za kuchukua ili kutatua matatizo hayo.

**Mchakato**

1. Toa utangulizi wa kazi ya kufanya na elezea lengo la kikao hicho. Sisitiza kwamba kikao hicho kitaangalia kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia kama sababu ya ukeketaji na mila zingine ambazo zinasababisha madhara kwa jamii.
2. Waulize washiriki kuwa ukeketaji ni nini na kwa nini unafanyika. Je, unafikiri kuna faida au hasara ya ukeketaji?
3. Gawanya washiriki katika makundi 2, na waambie wajadili kwa dakika 10:
   a. Kundi I: Matokeo ya Ukeketaji
   b. Kundi II: Mikakati ya Kuzuia Ukeketaji katika jamii yao.
4. Baada ya dakika 10 waambie watoe majibu yao. Tumia maswali yafuatayo ili kuchochea majadiliano zaidi:
   a. Je, wanajisikiaje kujadili mambo yanayohusiana na Ukeketaji?
   b. Ni kwa namna gani madhara ya Ukeketaji yanaathiri wasichana sawa sawa na wanawake katika jamii?
   c. Ni ujumbe gani katika jamii ambao unahimiza Ukeketaji katika jamii?
   d. Ni kitu gani ambacho kinasababisha kuwa na ugumu katika kuachana na Ukeketaji? Ni kwa namna gani hali hii inahusiana na uwezo wa kimadaraka?

**Muhtasari wa Kufunga**

Aina ya maisha, tamaduni na masuala ya dini, hutumika kuhakikisha kuwa wasichana wanakuwa bikira na waaminifu kabla ya kuolewa. Vitu kama ndoa za mapema, za kulazimishwa na za watoto, kutakasa wajane, kupima bikira na ukeketaji vinaruhusu kumiliki wanawake na wasichana kwa kuwazuia kujihusisha na ngono za mapema.

Mabadiliko yoyote katika Imani na hali za kijamii za kukeketwa au kutokukeketwa zinaweza kujitokeza tu pale iwapo sababu za kutokuwa na usawa wa kijinsia na matarajio ya kijamii kuhusu ukeketaji yatashughulikiwa. Hata hivyo, kukabiliana na sababu hizo kwa njia ya uwazi sana inaweza kusababisha mgongano mkubwa na kuweza kuendelezwa zaidi.

Kwa wanawake wengi, kukubalika katika jamii kupitia ukeketaji kunawafanya kutokuona athari zinazoambatana na ukeketaji, kwa sabau hiyo akina mama wanaendelea kuwakeketa watoto wao wa kike. Wengine wanajikuta kwamba wanafuata matakwa ya jamii kwa kufahamu au kwa kutokufahamu na wanaendeleza mategemeo hayo, mtizamo huo na tabia hizo.

Matokeo yake, mabadiliko ya nguvu ya ukeketaji inazidisha ugumu kwasababu wanawake na wanaume wanahusika katika kuendeleza mambo

hayo. Hivyo, umakini katika programu za jinsia unahitajika ili kuweza kuondoa ugumu uliopo.

## MADA YA 6: Mimba za Utotoni

### Malengo

Baada ya mada hii, washiriki wanategemewa kuwa na uwezo wa:

1. Kuelezea maana ya mimba za utotoni.
2. Kufafanua kwa nini wasichana wadogo wanapata mimba zisizotarajiwa.
3. Kuainisha athari zinazoambatana na mimba za utotoni ikiwemo athari za kimwili, kisaikolojia na kiuchumi.
4. Kuonesha mikakati ya kutokomeza mimba za utotoni.

### Mchakato

- Elezea kuwa kwa kawaida mimba za utotoni ni zile ambazo hazikupangwa ambapo wasichana wadogo wanazipata. Katika umri huo mwili haujakomaa vya kutosha kwa ajili ya kubeba mimba na kujifungua.
- Gawa washiriki katika makundi manne. Kila kundi lijadili yafuatayo:
    - ❖ Kundi 1: Sababu zinazochangia mimba za utotoni
    - ❖ Kundi 2: Sababu za kiafya za kuepuka mimba za utotoni

    - ❖ Kundi 3: Baadhi ya sababu za kijamii za kuepuka mimba za utotoni
    - ❖ Kundi 4: Njia za kuondokana na mimba za utotoni
- Makundi yawasilishe taarifa za majadiliano yao.
- Fupisha kwa kuwajulisha washiriki kuwa:
    - ❖ Katika matukio mengi, mimba za utotoni husababishwa na utegemezi wa kiuchumi na maisha magumu.
    - ❖ Fafanua kuwa iwapo msichana hana nguvu za kiuchumi, anaweza kujifunza kutoka kwa mtu mwingine ili kupata msaada, na huyo mtu mwingine anaweza kutumia mwanya huo kwa faida zake binafsi.
    - ❖ Endelea kueleza kuwa msukumo wa makundi rika kutoka kwa watu ambao wako karibu naye (anaowafahamu), na hata msukumo kutoka kwa wazazi, ngono za kulazimishwa kama kubakwa zinaweza kuwa sababu za mimba za utotoni.
    - ❖ Elezea kuwa mwanamke ambaye ana umri chini ya miaka16 mwili wake bado haujakomaa na hivyo nyonga yake bado ni ndogo na inaweza kusababisha uzazi wa shida pamoja na kusababisha matatizo ya kiafya au hata kifo kwa mama na mtoto. Fafanua kuwa kwa sababu ya umri mdogo, wanawake wanaopata watoto kwa mara ya kwanza wako katika

hatari kubwa ya kupata matatizo ya uzazi kama fistula ikilinganishwa na wale ambao wameshawahi kujifungua. Pia, vifo vya watoto wachanga mara nyingi vinatokea zaidi kwa wazazi wenye umri mdogo ikilinganishwa na wazazi waliokomaa.

- Sisitiza kuwa wanawake wadogo hasa wa umri chini ya miaka 15 wapo katika hatari ya kupata watoto njiti ikilinganishwa na wazazi ambao wana umri wa miaka 20 na zaidi. Pia, wanawake watoto wanapata athari za kuharibika mimba na kujifungua watoto ambao wamekwisha kufa kwa sababu uzazi wa kwanza ni hatarishi ikilinganishwa na uzazi unaofuatia.
- Wajulishe washiriki kuwa ni muhimu kuepuka mimba za utotoni kwa kuwa iwapo wanawake watasubiri hadi kufikia muda muafaka, wanakuwa na fursa ya kuendelea na masomo, kufanya kazi nje ya nyumbani na kufikia malengo yao ya baadaye. Pia, watu wanapochelewa kupata watoto inamaanisha kuwa na familia ndogo na inasaidia kuwa na faida za kiuchumi.

- Hitimisha kwamba, wasichana wajawazito wanaweza kuacha shule na wasichana wachache tu ndio wanaweza kurudi shule

baadaye. Jukumu la kulea mtoto pamoja na elimu ndogo inapunguza nafasi za kazi kwa wanawake wadogo na fursa za kupata kipato na mara nyingi wanawake wadogo wanajikuta wakikataliwa na baba wa mtoto na familia zao.

- Mwisho kabisa waeleze washiriki kuwa wavulana na wasichana wanaweza kuepuka mimba za utotoni kwa kufanya yafuatayo:
    - ❖ Kutokufanya ngono
    - ❖ Kutumia kondomu kila wakati kwa usahihi
    - ❖ Kutumia vidonge vya mpango wa uzazi kwa usahihi (waende vituo vya afya wapate ushauri)
    - ❖ Kuchelewa kujishughulisha na kujamiiana
    - ❖ Kujiepusha na makundi rika yanahamasisha kufanya ngono
    - ❖ Kataa kuingia katika ndoa za utotoni
    - ❖ Ikiwa msichana amelazimishwa kufanya ngono au amebakwa, awahi kufika katika kituo cha afya ili apatiwe huduma za matibabu ikiwa ni pamoja na dawa za kuzuia mimba, kupimwa maambukizi ya VVU, kupatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na ushauri nasaha pamoja na kuunganishwa na huduma za polisi.

## MADA YA 7: Nguvu ya Matembezi (Inafaa Zaidi kwa Vijana)

### Malengo

Mwisho wa majadiliano, washiriki wataweza kufanya yafuatayo:

1. Kuchunguza mabadiliko ya madaraka katika jamii.
2. Kuongeza uelewa wao wa namna ambavyo madaraka yalivyotengeneza hatima ya maisha na uzoefu wao.

### Kwa Ujumla: Nguvu ya Matembezi

1. Waambie washiriki kuwa wataendelea kwa kucheza mchezo. Waambie watu 12 wajitolee (sita wanaume na sita wanawake) kuja mbele ya chumba cha mkutano, wape uhusika kama ifuatavyo: [(Wahusika wa kiume: Mbunge, Mkulima mdogo ambaye ni mgane, Baba mwenye mtoto wa mwaka mmoja, Mwanafunzi, Mwanaume mwenye ulemavu na Dereva); na (Wahusika wa kike: Mama mwenye mtoto wa mwaka mmoja, Mjane, Mwanafunzi, Mfanyabiashara ya ngono, Mjasiriamali na Mwanamke mwenye ulemavu)].
2. Waambie hao waliojitolea kuja mbele wasimame katika mstari, bega kwa bega. Eleza kuwa utasoma sentensi chache. Kama wanafikiri kuwa mwanaume au mwanamke kunawawezesha kufanya kile kilichoelezewa

kwenye sentensi, wanakwenda hatua moja mbele. Kama hawana uhakika wanasimama pale walipo.

3. Waambie wakumbuke kuwa wao ni wawakilishi wa wasichana na wavulana. Kwa hiyo wanapofikiria kuhusu sentensi zile, ni lazima wafikiri jinsi ambavyo wasichana na wavulana wanavyoishi na kufanya shughuli zao kwa ujumla. Wasijibu kwa kuangalia mawazo/uelewa wao binafsi.
4. Hakikisha kuwa hakuna swali. Wakumbushe washiriki kuwa hili ni zoezi la kimya.
5. Mara utakapokuwa na uhakika kuwa washiriki wameelewa maelekezo, anza mchezo kwa kusoma sentensi zifuatazo:
    a. Ninaweza kuwa nje ya nyumbani hata baada ya saa 1 jioni;
    b. Sipiki chakula;
    c. Ninaweza nikafanya utani sehemu ya umma kuhusu jinsi nyingine na jamii ikajisikia ni sawa;
    d. Sitarajii kusaidia familia yangu nikiwa mkubwa;
    e. Ninaweza nikampiga mwenzi wangu na watu wasikasirike au wakakasirika kidogo;
    f. Ninaweza kuamka kwa kuchelewa wakati wa likizo;

g. Ninaweza kukaa kwa muda mrefu/uliopitiliza katika nyumba ya rafiki yangu;
h. Nilitiwa moyo kufanya shughuli nilizozichagua kwa sababu ya jinsi yangu;
i. Ninaweza kutoa mawazo yangu kwa uhuru;
j. Sina jukumu la kuwatunza wadogo zangu wa kike au wa kiume;
k. Ninaweza kwenda shule hata kama familia yangu ina fedha kidogo;
l. Ninaweza kucheka kwa sauti;
m. Ninaweza kuongea kwa sauti kubwa nyumbani; na
n. Ninaweza kucheza michezo nje ya nyumbani.

Baada ya kusoma kila sentensi tulia na waambie washiriki wabaki mahali walipo. Kama baadhi ya washiriki bado wameshikana mikono, wanaweza sasa wakaachiana.

Waambie washiriki waangaalie ndani ya ukumbi ili waone mahali waliposimama na mahali wengine waliposimama. Waambie wachukue hatua ya kutafakari juu ya nafasi zao wenyewe na nafasi za wengine katika maisha.

Mwisho wakusanye kila mmoja katika duara kubwa na rudia kwa kifupi kuwaeleza hili zoezi. Hakikisha kuwa wanaume na wanawake wanatoa mawazo yao na kila mtu anajisikia kuwa salama na ameheshimiwa wakati wote wa majadiliano kwa kuuliza:

- Unajisikiaje kwa kufanya hili zoezi?
- Ulikuwa unajisikiaje mwanzoni wakati wote mlipokuwa katika mstari?
- Ulijisikiaje uliposogea mbele? Uliporudi nyuma?
- Umejisikiaje ulipoachia mkono wa jirani yako?
- Umeona nini kimetokea kwa wengine wakati zoezi lilipokuwa linaendelea?" (Dadisi: "Je, katika mwendelezo wa mchezo kulikuwa na mabadiliko kutoka katika mchezo na kuwa kitu halisi chenye mantiki?")
- Unafikiri nini au unajisikiaje wakati ulipoona kila mtu alipokuwa amesimama mwisho wa mchezo? Kuna jambo lolote ambalo lilikushangaza kutokana na sehemu watu walizokuwa? Ni nani alikuwa ametangulia na ni nani alikuwa amesimama mwisho wakati wa mchezo?
- Kuna yeyote kati yenu ambaye alirekebisha ukubwa wa hatua zake (mfano, kupunguza hatua) kadiri mchezo ulipokuwa unaendelea? Kwa nini?

- Kuna yeyote kati yenu ambaye alichagua kutokuwa mkweli wakati wa zoezi hili? Kwa nini? Hii inatufundisha nini kulingana na uzoefu wetu? (Dadisi: “Kuna aibu au unyanyapaaji ambao upo kati yetu kulingana na uzoefu wa kutafuta madaraka?”)
- Je, ulijisikiaje mwanzoni wakati nilipokuambia kukimbia kwenda ukutani? (Michango inaweza kujumuisha: mbali sana, karibu sana, ilikuwa vigumu kukimbia, nilijua sitashinda, sababu ilikuwa nini, n.k.)
- Je, zoezi hili linatufundisha nini kuhusu kutokuwa na usawa wa madaraka kati ya wanawake na wanaume?
- Umejifunza nini kuhusu uwezo wako binafsi? Je, uwezo wa wale wanaokuzunguka?

**Malizia Kipindi kwa Muhtasari Ufuatao:**

- Katika jamii yetu, kwa kawaida wanawake wanakuwa na madaraka ya chini kuliko wanaume. Hili ni jambo la kimila-kitu ambacho kinaonekana kuwa ni kawaida katika jamii yetu, lakini inaweza ikabadilika iwapo watu wengi wataamini katika mabadiliko.
- Kutokuwa na usawa katika madaraka kati ya wanawake na wanaume inamaanisha kwamba wanawake wanakuwa katika nafasi duni/ambayo haina faida kwake hasa

kuanzia kwa wasichana, katika kaya, jamii na Taifa kwa ujumla.

- Ukatili dhidi ya wanawake ni njia mojawapo inayosababisha muendelezo wa kutokuwa na usawa wa madaraka.
- Inakuwa sio sahihi kwamba wanawake na wanaume hawaendi mbele wakiwa katika usawa wa maisha.

**Muhtasari wa Kufunga**

Wasichana na wavulana wanaweza kutofautiana lakini hii isisababishe kutokuwa na usawa kati yao. Kuzaliwa Mvulana au msichana kusisababishe kuwa na tofauti kwa namna ambayo wanathaminiwa na kupewa uzito sawa. Lakini kwa ukweli wasichana na wavulana wanakuwa na tofauti katika kupata haki zao za msingi na pia kuna tofauti kati ya uhuru anaopewa mvulana na ule anaopewa msichana.

Haki za msingi za kijinsia zinaweza kusababisha tofauti katika madaraka. Tunapokuwa na makatazo ya kijamii zaidi inaambatana na kuwa na uwezo wa chini katika kufanya maamuzi na katika kuchukua hatua.

**Wasichana wana haki ya kuwa na uwezo wa madaraka! Wasichana wana haki ya kufanya maamuzi ambayo yanagusa maisha yao!**

## MADA YA 8: Kuvuka Mto – Kushughulikia Mila Hasi za Kijinsia

### Lengo

Ifikapo mwisho wa majadiliano, washiriki watakuwa na uwezo wa kuelewa zoezi la kuvuka mto ambalo linaweza kutumika katika kushirikisha jamii juu ya mila za kijinsia.

### Ufafanuzi Mfupi

Katika kuvuka mto, hadithi inayoelezewa imekuwa ikitumika ili kutenganisha kundi la wanajamii kama ambavyo waliambiwa kufanya uamuzi unaohusisha jinsia, jinsi, na ukatili wa kijinsia. Zoezi hili linachunguza nafasi ya wanawake na wasichana katika jamii na jinsi ambavyo mila hasi za kijinsia zinavyoathiri mtazamo wetu wa madaraka au uwezo wa wanawake na wasichana. Kazi hii inatoa changamoto kwa washiriki ili waweze kuchunguza mila hasi za kijinsia ambazo zinakumbatiwa na kuendelezwa katika jamii.

### Kabla ya Kuanza

Soma kwa uangalifu hadithi ya Kuvuka Mto na waza kuiweka katika hali mahsusi ya kwako wewe na mada ambayo unataka kushirikisha jamii.

### Kwa Kuanza

- Tambulisha zoezi linalokwenda kufanyika na lengo la hadithi ya kuvuka mto.

- Waambie washiriki wote kujiunga katika duara kubwa na waambie wafunge macho.
- Eleza kuwa utasoma hadithi, ambayo itaonyesha mwelekeo wa hali halisi ambayo inaweza kutokea katika jamii yao, na utawaambia wafanye maamuzi kutokana na mhusika wa hadithi hiyo. Elezea kuwa utajadili uchaguzi wao baadae.

**Soma hadithi ifuatayo kwa kundi:**

*Mwanamke anakwenda kununua mbogamboga kila siku kutoka katika soko ambalo ni la kuvuka mto, na anarudi nyumbani kwa mume wake. Siku moja alivuka mto ili kwenda kununua mboga mboga na akapendana na mtu mwingine. Baada ya kukutana na huyo mtu, aliendelea kwenda sokoni kila siku na kurudi kwa mume wake. Siku moja kulikuwa na mvua iliyoambatana na radi kubwa, ikasababisha ule mto kufurika na hakuweza kurudi nyumbani kwa kushindwa kuvuka ule mto kwa kupita juu ya mawe/miamba ili afike nyumbani kwa mume wake kama ilivyokuwa kawaida yake. Kwa kuwa ilianza kuwa giza, yule mwanamke alikuwa na mambo matatu ya kuchagua:*

- *Aogelee katika maji yaliyokuwa yanazunguka, yalikuwa yanakwenda kwa kasi, lakini kuna uwezekano mkubwa wa yeye kufa;*

- *Kuna nahodha wa boti ambaye anaweza kumvusha katika mto, lakini atafanya hivyo iwapo tu atakubali kufanya ngono na yeye kwanza; na*
- *Anaweza akatembea kwa kutembea kufuata njia ambayo inapita katika msitu, lakini kulikuwa na mwanaume ambaye anajulikana kuwa ni mbakaji ndani ya ule msitu, na pengine angembaka.*

**Waulize washiriki:**

- Kama wewe ungekuwa ni huyo mwanamke, ungechagua uamuzi upi na kwa nini?
- Ungesema nini ili kuwashawishi wengine ili wakubaliane na maamuzi yako?
- Uliza: "Kama huyu mwanamke angekuwa mkeo au mtoto wako wa kike, ungemchagulia uamuzi upi na kwa nini?"
- Je, hadithi hii inahusiana vipi na maisha yetu ya kawaida?

**Waeleze washiriki kuwa:**

- Chaguzi hizi zinafanana na zile ambazo tunafanya katika maisha halisi na kwamba hakuna uchaguzi wowote kati ya hizo ambao ni sahihi zaidi au ni wa moja kwa moja na mara nyingi umefungamana na mambo ya jinsia na majukumu ya kijinsia.

- Katika baadhi ya tamaduni na jamii, heshima, uaminifu na misingi ya mwanamke vinahesabiwa kuwa na umuhimu sana kuliko hata uhai/maisha yake.
- Waambie washiriki watafakari: Je, inaweza kuwa sahihi kwa mwanamke kumwambia mume wake kuwa amebakwa, kuliko kumwambia kuwa alikubali kufanya ngono ili aweze kuokoa maisha yake?

**Waambie washiriki watafakari tena:**

- Je, kama tukigeuza hii hadithi na kuwa ni mwanaume ambaye alitakiwa avuke mto, Je, mawazo/mategemeo yetu yangebadilika? Je, mwanaume angefikiria kurukia katika maji? Au angekubali kuingia katika hatari ya kulawitiwa?
- Umejifunza nini kupitia hadithi hii?
- Funga mjadala kwa kushukuru washiriki kwa mawazo na michango yao.

## MADA YA 9: Mahusiano Mazuri na Mabaya Kiafya (Healthy and Unhealthy Relationships)

### Lengo

Baada ya majadiliano, washiriki wataweza kuainisha tabia nzuri na mbaya ambazo ziko katika mahusiano.

**Mchakato**

1. Kabla ya zoezi, andika yafuatayo kwa maandishi makubwa katika vipande vya karatasi: “Mazuri Kiafya,” “Mabaya Kiafya” na “Inategemea”.
2. Pia andika hali ya kila aina ya uhusiano katika kadi tofauti (au kipande cha karatasi):
    - Kitu muhimu zaidi katika mahusiano ni ngono.
    - Huwezi kutokukubaliana na mwenzi wako.
    - Unatumia muda wako mwingi peke yako bila mwenzi wako.
    - Unajisikia raha kuwa na mwenzi wako.
    - Mwenzi wako bado yuko karibu sana na rafiki yake wa kike/kiume wa zamani.
    - Unakuwa na ukaribu zaidi na mwenzi kadiri mnavyoishi muda mrefu.
    - Utafanya kitu chochote kwa ajili ya mwenzi wako.
    - Habari ya ngono/tendo la ndoa halizungumziwi.
    - Mtu mmoja ndiye ambaye anafanya maamuzi yote kwa mwenzi/wenzi.
    - Unakuwa katika mahusiano kwa sababu ni bora kuliko kuishi peke yako.
    - Una uwezo wa kuamua chochote unachotaka kufanya.

- Mtu mmoja anaweza kumpiga mwingine ili kumfanya huyo mwanaume/mwanamke kutii.
- Mnaongelea matatizo pale ambapo yanajitokeza katika mahusiano.
- Mnagombana na kupigana mara kwa mara.

Kama hauna kadi/karatasi, unaweza kurahisisha kwa kusoma kwa sauti kila hali kwa washiriki.

**Ufupisho wa Mwezeshaji**

Katika mahusiano mazuri, wenzi wote wanakuwa na furaha kuwa pamoja. Katika mahusiano mabaya, mwenzi mmoja au wote wanakuwa hawana furaha kwa sababu ya matatizo yanayoendelea katika uhusiano wao ambayo hayajatatuliwa. Masuala ya kijinsia yanachangia kumfanya watu kukaa katika mahusiano ambayo sio mazuri. Kwa ujumla wanawake wanajikuta katika wakati mgumu kuondoka na kuachana na mahusiano mabaya kuliko wanaume. Wanawake hupata kiasi kidogo cha fedha ukilinganisha na wanaume na wanamiliki kwa kiwango kidogo rasilimali za kiuchumi kama vile ardhi. Hii huwafanya wanawake wengi kutegemea waume zao kiuchumi. Kijamii, wanawake wengi hunyanyapaliwa kwa kuachwa na waume zao.

Kuna msukumo wa kijamii unaowafanya wanawake waendelee kubaki katika ndoa kwa ajili ya familia.

Wanaume wanahitaji ujuzi wa namna ya kuongea na wake zao au marafiki zao wa kike kuhusu kutengeneza mahusiano mazuri. Kuna kusaidiwa kidogo kwa wanaume au wanawake katika kuleta mahusianao mazuri. Lakini sheria za jinsia kwa mwanamke huwaruhusu kupata msaada wa namna wanavyojisikia. Sheria za jinsia kwa wanaume huwa ngumu kwa wao kupata msaada kwa masuala yanayowasibu au kuonesha namna wanavyojisikia. Hatua ya kwanza ili kupata mahusiano mazuri ni kuzikataa/kupinga hizo mila hasi za jinsia. Wanaume wanahitaji fursa nyingi zaidi na ruhusa/uhuru kwa ajili ya kupata msaada. Wanaume wanahitaji pia mafunzo ya namna ya kusema yale yanayowasibu katika mahusiano.

**Mchakato**

1. Katika ukuta mbele ya kundi, weka neno “mbaya” upande wa kushoto na neno “nzuri” upande wa kulia. Elezea kuwa hii ni tofauti kati ya tabia za mahusiano ambazo tutazijadili. Weka wazi kuwa mahusiano mazuri yanaweza kuwepo mahali popote kati ya kuwa mazuri au mabaya.
2. Weka kundi katika watu wawili wawili. Mwambie kila mtu na mwenzake mfano wa mahusiano mazuri na mahusiano mabaya.

Mifano inaweza kutokana na maisha yao wenyewe au kutoka kwa watu wanaowafahamu. Mpe kila mmoja dakika tano za kushirikishana mifano yao.

3. Wakusanye wote pamoja. Waambie makundi kuelezea mahusiano mazuri na mahusiano mabaya. Shirikisha maelezo yao na yale yaliyotolewa na mwezeshaji. Waambie kundi kubungua bongo kuhusu mahusiano yenye ubora. Andika maelezo hayo chini ya neno “zuri”. Sisitiza mambo ya msingi ya ubora: heshima, usawa, kuwajibika na uwazi/ukweli/uaminifu. Eleza kwa uwazi kwamba mahusiano mabaya ni kinyume cha hayo yaliyo mazuri.
4. Weka neno “inategemea” katika lile eneo la mahusiano, alafu elezea “Hali ya Uhusiano” katika kadi, wape washiriki. Chagua mshiriki mmoja asome kwa sauti yaliyoandikwa katika kadi. Waambie waeleze ni namna gani uhusiano mzuri au mbaya katika hali hiyo ulivyo na ni kwa nini wanafikiri hivyo. Waambie waweke kadi zao katika sehemu sahihi kulingana na uhusiano ulioandikwa au waweke sehemu ya “inategemea”.
5. Uliza kundi wanafikiri nini kulingana na sehemu walizoweka kadi, wape muda wa kujadili. Iwapo hawakubaliani, wakumbushe juu ya ubora wa mahusiano mazuri ambayo ni (heshima, usawa,

kuwajibika, uaminifu). Waulize iwapo hali hiyo inaonesha ubora.

6. Rudia sehemu ya 4 na 5 katika kila hali ya kila uhusiano ambao upo kwenye kadi.
7. Endesha majadiliano ya ujumla kwa kuuliza maswali yafuatayo:
   a. Kwa nini unafikiri watu wengine wanakuwa na mahusiano mabaya?
   b. Je, sababu zinatofautiana kati ya wanawake na wanaume? Kwa nini?
   c. Ni kwa namna gani marafiki au familia zinaweza kusaidia watu wenye mahusiano mabaya?
   d. Ni ujuzi gani na msaada upi ambao unahitajika kwa ajili ya kuwasaidia wanaume ili wawe na mahusiano mazuri na wenzi wao?

**Muhtasari wa Kufunga**

Mahusiano mazuri yanategemea uwepo wa mawasiliano mazuri na kuheshimiana kati ya pande zote. Maamuzi yafanyike kwa pamoja na kusiwe na upande ambao unatawala maamuzi katika mahusiano. Mahusiano ambayo sio mazuri kwa upande mwingine huweza kusababishwa na mawasilano mabaya, na kutokuwa na usawa katika kufanya maamuzi, ambayo yanasababisha kukosekana kwa mazungumzo ya wazi kuhusu tabia ya kufanya tendo la ndoa/ngono na uzazi wa mpango kuwa jambo gumu sana, matokeo yake ni

kuwafanya wenzi au mwenzi mmoja kuwa katika hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa na VVU.

## MADA 10: Aina Mpya za Ujasiri - Kusimama Imara Dhidi ya Uhusiano Usiofaa na Unyanyasaji wa Kijinsia

### Malengo

Hadi kufikia mwisho wa majadiliano haya mshiriki ataweza:

1. Kutambua mikakati inayokuza mahusiano mazuri.
2. Kuhimiza mikakati inayokuza mahusiano mazuri.
3. Kuelewa njia za kuendeleza mahusiano mazuri ya kingono yenye haki na uwajibikaji zaidi.
4. Kuelewa njia nzuri za kuwajibika ili kukabiliana na changamoto za ukatili wa wanaume dhidi ya wanawake au ukatili wa wanawake dhidi ya wanaume.

### Maandalizi ya Awali

Kabla ya kipindi kuanza, tengeneza "Kibao cha Ujasiri" kwenye ukuta katika chumba cha mafunzo kwa kuweka alama ya "Ujasiri Mdogo" upande wa kushoto wa chumba na alama ya "Ujasiri Zaidi" upande wa kulia.

**Matukio ya Vitendo**

- Puuza sherehe za ukeketaji zinazofanyika mtaani mbele ya nyumba yako.
- Mwambie mwalimu wa taaluma kwamba mwalimu wako mkuu wa shule amekufuatilia kwa ajili ya mapenzi.
- Mwambie baba yako kwamba mjomba wako amekuwa akija chumbani kwako usiku kukuomba mfanye naye tendo la ngono.
- Piga simu Polisi na uwaambie kuwa rafiki yako wa karibu au jamaa yako anakeketwa.
- Je, unaweza kuwa shahidi dhidi ya wazazi wako wanaotaka kukuozesha kabla ya kumaliza shule yako ya sekondari?
- Tetea haki za msichana unapokuwa na marafiki zako kwenye baa.
- Nenda kwa mwanaume na umwambie aache kumnyanyasa kingono binti wa jirani yako anayepita.
- Mwambie Afisa wa Polisi kwamba aache kumnyanyasa kingono msichana anayepita.
- Zungumza na binti yako au mwanao kuhusu kutumia kondomu.
- Kukataa kuolewa hata kama wazazi wako wanakulazimisha.
- Kumwambia jirani yako kwamba hawapi haki watoto wake kufanya maamuzi.
- Chukua muda kumsaidia jirani aliyenyanyaswa kingono.

- Uwe na uwezo wa kuimba sokoni kuhusu vitendo vya ukeketaji na madhara yake.
- Uweze kuwatembelea viongozi wa kimila katika Kijiji chako na kuwaambia waache kuwaozesha wasichana walio chini ya miaka 18.
- Kusimama mbele ya ibada msikitini au kanisani na kusema kwamba kuwaozesha wasichana walio chini ya miaka 18 huleta athari za kijamii, kiuchumi na kiafya.
- Kumwambia bosi wako kwamba hupendi tabia zake za kutongoza kila msichana mpya anayekuja kwa nafasi ya kazi.
- Lia hadharani unapojisikia kulia.

**Hatua Muhimu**

1. Kwa kuanza, waulize washiriki kwa nini wanafikiri wanaume wanapaswa kuona kuwa wanahusika na wanawajibika kuhusiana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Wakati wa majadiliano, pitia mambo makuu na uhakikishe kwamba yameshughulikiwa.
2. Kisha, waambie kundi watengeneze orodha fupi ya hatua ambazo wanaume wanaweza kuchukua ili kuzuia unyanyasaji, hasa dhidi ya wanawake na watoto, na kukuza usawa wa kijinsia katika mahusiano yao na katika jamii kwa ujumla. Andika masuala hayo kwenye bango.
3. Wape washiriki kadi.

4. Waombe washiriki kuchunguza hali zifuatazo na kubainisha ni wapi zinaangukia kwenye kibao cha “Ujasiri Mdogo - Ujasiri Zaidi” uliobandikwa ukutani.
5. Baada ya kadi zote kubandikwa ukutani, pitia kila moja na jadili na kundi zima kama wanakubaliana na uwekaji wa kadi hizo au la.

**Ujumbe wa Kufungia Kipindi**

Ili mahusiano yawe na afya, kuna haja ya kuhakikisha kuwa kunakuwa na usawa na uwajibikaji zaidi kwa wenzi wote wawili (mume na mke). Hili linaweza kupatikana kwa kuheshimiana, maamuzi ya kirafiki na mawasiliano mazuri kati ya wanandoa bila mmoja kuhatarisha uhuru wa mwingine kwani kufanya maamuzi yasiyo sawa kunaweza kusababisha uhusiano mbaya hivyo kuongeza tabia za hatari kwa familia.

**KIAMBATISHO NA. 3: FOMU YA KUTOA TAARIFA YA MAJADILIANO NGAZI YA JAMII (FOMU NA. 1)**

| |
|---|
| **Tarehe: ---------------------------**<br><br>**Jina la Mwezeshaji: -----------------------------------------** |
| **Jina la Taasisi inayoendesha Majadiliano ya Jamii:**<br>**………………………………………..** |
| **Mahali ambapo Majadiliano ya Jamii yamefanyika:**<br>• Ukumbi: ……………………………………….<br>• Kata: ……………………………………….<br>• Wilaya: ……………………………………….<br>• Mkoa: ………………………………………. |
| **Utangulizi** *(Utangulizi kuhusu majadiliano ya Ngazi ya Jamii, idadi ya washiriki, taarifa za kina zinazoonesha mahali/ukumbi, na taarifa zinazoonesha jinsi, umri, hali ya uchumi (kama itahitajika)).* |
| **Mila na Desturi za Jamii ambazo Zimejadiliwa** *(Toa maelezo mafupi kuhusu mila na desturi muhimu ambazo zilikuwa ni kiini cha majadiliano*). |
| **Taarifa za Kazi** *(Elezea kwa kifupi kazi ambazo zimefanyika wakati wa majadiliano na ainisha njia na mbinu zilizotumika wakati wa majadiliano).* |
| **Malengo ya Kazi** *(Elezea kwa kifupi lengo la Majadiliano ya Kijamii).* |
| **Ufupisho wa Mafanikio ya Mjadala** *(Tafadhali toa* |

| |
|---|
| *maelezo ya kuhusu mafanikio katika kila lengo la mjadala).* |
| **Changamoto Zilizojitokeza** *(Tafadhali elezea changamoto/ugumu wowote ambao ulijitokeza wakati wa majadiliano na ni hatua zipi zilichukuliwa ili kutatua changamoto hizo).* |
| **Mambo Mazuri Yaliyojitokeza na Yanayofaa Kuigwa** *(Tafadhali tumia sehemu hii kuonesha mambo mazuri yaliyojitokeza na mambo waliyojifunza washiriki yanayohusiana na majadiliano ya kijamii. Pia elezea mambo waliyojifunza kutokana na majadiliano hayo, na eleza mikakati au njia ambazo hazikufanikiwa kama ilivyotarajiwa na kwa nini?).* |
| **Mrejesho wa Mwezeshaji** *(Tafadhali toa mrejesho na ushauri kuhusu uendeshaji wa majadiliano ya kijamii ili kuboresha programu hizi kwa siku zijazo).* |
| **Kwa Matumizi ya Ofisi tu**<br>Tarehe ya Kupokea Taarifa: --------------------------------<br><br>Imepokelewa na Kupitishwa na: ………………………..<br><br>Cheo: ……………………………………………………<br><br>Sahihi: ------------------------------------------------------ |

**KIAMBATISHO NA. 4: FOMU YA MPANGO KAZI WA JAMII (FOMU NA. 2)**

| NA. | ENEO LA KIPAUMBELE | KAZI | MHUSIKA/SHIRIKA | TAREHE YA KUKAMILISHA | RASILIMALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukeketaji | Kutengeneza Sheria ndogo za Jamii kwa ajili ya kuzuia ukeketaji | Kamati ya Kata | Hadi Januari 2022 | Muda wa Mikutano, Fedha, Watu |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |
| 5 | | | | | |

## KIAMBATISHO NA. 5: TATHMINI KABLA NA BAADA YA MAJADILIANO

Ufuatiliaji na tathmini ni muhimu kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa majadiliano ngazi ya jamii kwa kuwa inaruhusu watekelezaji au waandaaji kufanya maamuzi yanayofaa siku hadi siku na kuhakikisha kwamba afua zinatekelezwa kama zilivyoandaliwa na kurekebisha pale inapobidi.

Tathmini huwawezesha watekelezaji au waandaaji wa majadiliano ngazi ya jamii kuelewa na kuonesha matokeo tarajiwa ya kazi yao, kuamua juu ya mikakati bora ya kufikia malengo na kuandika mafunzo waliyojifunza ili kuboresha majadiliano kwa siku zijazo. Kwa hiyo, inashauriwa kuwa kuna umuhimu wa kufanya tathmini kabla na baada ya majadiliano kwa vipindi vya majadiliano ngazi ya jamii vinavyochunguza mila na desturi zinazochangia ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa washiriki wanaojua kusoma na kuandika na wale wasiojua kusoma na kuandika. Utaratibu huu utawapa washiriki wote fursa ya kutoa maoni na mtazamo wao kuhusu jinsi majadiliano hayo yatakavyoendeshwa/yalivyoendeshwa kwa ujumla. Pia, tathmini huwapa wawezeshaji fursa ya kuelewa endapo wameeleweka vyema katika kuwafikia walengwa waliokusudiwa. Hili linaweza kufanyika

kupitia madodoso, mahojiano au mijadala ya kikundi. Zifuatazo ni Fomu kwa ajili ya kufanyia Tathmini Kabla na Baada ya Majadiliano (**Fomu Na. 3A**) pamoja na kufanyia Tathmini ya Mchakato wa Uwezeshaji wa Majadiliano Ngazi ya Jamii (**Fomu Na. 3B**):

**Fomu Na. 3A: Tathmini Kabla na Baada ya Majadiliano**

| Na. | Maswali | Tathmini (%) |
|---|---|---|
| 1. | (a) Unaelewa nini kuhusu mila na desturi chanya au nzuri<br>……………………………………………<br>……………………………………………<br>……………………………………………<br><br>(b) Unaelewa nini kuhusu mila na desturi zenye madhara<br><br>……………………………………………<br>……………………………………………<br>**(Alama 20)** | |
| 2. | (a) Taja mila na desturi chanya au nzuri zinazofaa kuendelezwa katika jamii yako:<br>(i) ……………………………………<br>(ii) ……………………………………<br>(iii) …………………………………… | |

| | | |
|---|---|---|
| | (b) Taja mila na desturi zenye madhara zinazotakiwa kutokomezwa katika jamii yako:<br>(i) ………………………………………<br>(ii) ……………………………………….<br>(iii) ……………………………………….<br>**(Alama 30)** | |
| 3. | Nani anayehusika katika kutokomeza mila na desturi zenye madhara katika jamii?<br>(i) ………………………………………<br>(ii) ………………………………………<br>(iii) ………………………………………<br>**(Alama 30)** | |
| 4. | Taja huduma muhimu anazotakiwa kupatiwa mwathirika wa ukatili unaosababishwa na mila na desturi zenye kuleta madhara katika jamii.<br>(i) ………………………………………<br>(ii) ………………………………………<br>(iii) ………………………………………<br>(iv) ………………………………………<br>**(Alama 20)** | |

**Fomu Na. 3B: Tathmini ya Mchakato wa Uwezeshaji wa Majadiliano Ngazi ya Jamii**

| Na. | Vigezo vya Tathmini | Ndiyo | Hapana | Sababu / Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Je, mada za majadiliano ziliwasilishwa vizuri? | | | |
| 2. | Je, washiriki walipewa nafasi sawa/fursa ya kutosha kutoa maoni yao? | | | |
| 3. | Je, majadiliano yamekuwa na manufaa kwako? | | | |
| 4. | Je, muda uliopangwa wa majadiliano unafikiri ni wa kutosha ukilinganisha na mada zilizotolewa? | | | |
| 5. | Je, ni wazo zuri kushiriki majadiliano kama haya na wanajamii wengine? | | | |